**MWINYI** alipotea Ulaya, aishiwa nauli, atembea
UKURASA 3



**RAIS** Mahakama ya Afrika aomba Tanzania kurejea
UKURASA 2



UKURASA 11


# Nipashe
MWANGA WA JAMII

Jumamosi Mei 22, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580588

www.ippmedia.com

The Guardian · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




SACP Camilius Wambura

Jimson Charles Kibiki

# Majambazi wamkaribisha RPC mpya Dar

**WAUA** kigogo Vodacom, wapora mamilioni... *Endelea Ukurasa 2*

UKURASA WA 3

## JK: MAKABURU NI CHANZO KITUO CHA POLISI SELANDER

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete amesimulia jinsi makaburu wa Afrika Kusini walivyosababisha kujengwa kwa Kituo cha Polisi Selander jijini Dar es Salaam...

## UPINZANI WAMJIBU KATIBU WA CCM

UKURASA 4

UKURASA WA 4

## MAKUSANYO MADENI YA MATREKTA YASUASUA

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, limesema kuwa limekusanya zaidi ya Sh. milioni 465.1 kati ya Sh. bilioni 5.2 za matrekta na zana za kilimo kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, yaliyokopwa...





Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alipowasili katika Semina ya Elimu ya Fedha na Uwekezaji iliyoandaliwa na benki hiyo, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC). Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay na Makamu Mwenyekiti, Prof. Neema Mori. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TRA yazifungua akaunti zilizofungwa madai kodi

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YAJIPANGA KUFANYA MAAJABU** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Rais Mahakama ya Afrika aomba Tanzania kurejea

**Na Christina Mwakangale**

MAHAKAMA ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, imesema ipo katika mazungumzo kuzishawishi nchi wanachama, ikiwamo Tanzania, kurejea katika utekelezaji wa azimio linaloruhusu wananchi pamoja na asasi zisizo za kiserikali, kupeleka malalamiko moja kwa moja mbele ya mahakama hiyo.

Tanzania ilijitoa rasmi Novemba 14, mwaka jana, baada ya notisi ya mwaka mmoja iliyotoa mwaka juzi, ikiungana na Rwanda pamoja na Ivory Coast kutotekeleza azimio hilo.

Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Jaji Sylvain Ore, akizungumza jana, baada ya kufanya ziara katika vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam, alisema Tanzania irejee kwenye utekelezaji wa azimio hilo katika mahakama hiyo, kwa kuwa ni mwenyeji na kesi nyingi zaidi kuliko mwanachama mwingine.

Azimio hilo linaeleza katika Ibara ya 34 (6) ya Mkataba unaoanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; Muda wowote baada ya nchi kuridhia mkataba inaweza kutoa Azimio la kukubali Mahakama kupokea malalamiko (kesi) kwa mujibu wa Ibara ya 5(3) ya Mkataba.

Kwamba; Na kwa maana hiyo Mahakama haitakuwa na uwezo wa kusikiliza malalamiko ama kesi itakayoletwa, kwa mujibu wa Ibara ya 5(3) endapo kesi hiyo inaihusu nchi ambayo haijaweka azimio.

Jaji Ore alisema kutokana na umuhimu wa mahakama hiyo kulinda haki za binadamu, ana imani Tanzania baada ya kuingia uongozi mpya, itafikiria namna ya kurejea kwenye utekelezaji wa azimio hilo.

"Hii ni mahakama ya kimataifa, tunafanya kazi kwa mujibu wa sheria na hatufanyi kazi kisiasa. Tunajitahidi kuunganisha nchi zaidi za Afrika kusiwapo na anayeachwa kando, kati ya wanachama 55 zinazotekeleza mkataba ni 31," alisema Jaji Ore.

Alisema umuhimu wa kurejea Tanzania kwenye mahakama ni pamoja na kuwa na kesi za asilimia 18 ya kesi zote zilizopo katika mahakama hiyo na ikizingatiwa mkataba iliyoingia pamoja na nchi nyingine.

"Mahakama ipo Arusha, imekuwa ikiendesha kesi mbalimbali kuhusu haki za binadamu tangu kuanzishwa kwake," alisema.

Kwa mujibu wa notisi iliyotolewa na kusainiwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa kipindi hicho, Prof. Palamagamba Kabudi, Tanzania imeamua kujitoa katika azimio iliyokuwa imeweka, kutokana na azimio hilo kutumika kinyume na mambo ambayo nchi iliyawekea mipaka.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na Mjumbe Maalum kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Burundi, Evariste Ndayishimiye, Balozi Ezechiel Nibigira ambaye ni Waziri anayeshughulikia Masuala ya Afrika Mashariki, Vijana, Michezo na Utamaduni wa Burundi, baada ya kuwasili Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Majambazi wamkaribisha RPC Dar

**Na Romana Mallya**

WATU wanaosadikiwa kuwa ni majambazi wamemuua Meneja Masoko na Mauzo wa Vodacom, Jimson Kibiki, kwa kumpiga risasi tumboni na kumpora Sh. milioni nne karibu na nyumbani kwake Mbezi Beach jijini Dar es Salaam baada ya kutoka benki.

Tukio hilo lilitokea juzi mchana, ikiwa ni siku mbili tangu Camilius Wambura ateuliwe kuwa Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, akichukua nafasi ya Lazaro Mambosasa aliyehamishiwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

Kamanda Wambura alithibitisha jana kuwapo kwa tukio hilo alipotafutwa na Nipashe na kubainisha kuwa hadi jana asubuhi, watu wawili walikuwa wanawashikilia kwa uchunguzi.

"Alivamiwa na watu wanaodhaniwa kuwa ni majambazi, walimpiga risasi na inasadikika walimpora Sh. milioni nne, tunaendelea na uchunguzi.

"Kwa sasa tunashikilia watu wawili ambao hatuwezi kutaja majina yao kwa sababu za kiuchunguzi," Kamanda Wambura alisema.

Alisisitiza ujumbe wake kwa majambazi kuwa watahakikisha wanawashughulikia kwa mujibu wa sheria kwa kuwatafuta, kukamata na kuzuia matukio hayo kutokea ndani ya mkoa huo wa kibiashara.

Mmoja wa majirani ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema kijana huyo alikutwa na umauti baada ya kutoka benki kuchukua fedha za kulipa kodi ya nyumba.

"Wakati akielekea benki alichukua bodaboda na wakati akirejea nyumbani, njiani akiwa amebeba fedha hizo kwenye bahasha, hatua chache karibu na nyumbani akavamiwa na watu hao na alipiga kelele kuomba msaada ndipo wakamfyatulia risasi," alidai.

Jirani huyo alidai kuwa baada ya Jimson kupigwa risasi na kuporwa fedha alizokuwa nazo, alipiga kelele kuomba msaada ndipo mke wake aliposikia na kwenda kumsaidia kumpeleka hospitalini.

Alidai kijana huyo alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mei 7, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akizungumza na wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam, alitoa onyo kwa majambazi na wahalifu wengine kwa kile alichokiita kupima kina cha maji.

Vilevile, wakati wa kuzindua kiwanda cha ushonaji wa sare za Jeshi la Polisi mkoani Dar es Salaam mwanzoni mwa wiki, Rais alisisitiza udhibiti wa ujambazi utakuwa miongoni mwa vigezo muhimu katika uteuzi na utenguzi wa makanda wa polisi.

# TRA sasa yazifungulia akaunti zote ilizofunga

**Na Joseph Mwendapole,**
MOROGORO

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imezifungulia akaunti zote za wafanyabiashara zilizokuwa zimeshikiliwa kutokana na madeni ya kodi.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alibainisha hayo jana wakati akitoa mada kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Jukwaa la Wahariri (TEF).

Alisema hivi sasa mamlaka hiyo inaingia mikataba ya makubaliano na wafanyabiashara hao wenye madeni ili walipe kwa utaratibu maalum.

Alisema sheria inairuhusu TRA kushikilia akaunti ya mtu yeyote ambaye ana deni la kodi kama njia ya kupata fedha ambazo serikali inadai.

Kayombo alisema uamuzi wa kushikilia akaunti ya mfanyabiashara huwa ni wa mwisho kabisa baada ya njia zingine zote kama majadiliano kushindikana.

"Si kawaida kushikilia akaunti ya mfanyabiashara na uamuzi huu mara nyingi unakuwa wa mwisho kabisa baada ya jitihada zingine kushindikana ikiwamo majadiliano na mhusika.

"Tumeamua kuziachia hizi akaunti ili sasa tuwe tunakaa mezani na kujadiliana na wafanyabiashara wenye madeni namna bora ya kulipa taratibu na tunaachana na ule wa kushikilia akaunti zao," alisema.

Kuhusu fedha zilizokuwa kwenye akaunti hizo, Kayombo alisema kama mhusika alikuwa akidaiwa na fedha hizo kukatwa na kupelekwa Benki Kuu (BoT), hatazipata.

Katika hotuba yake ya kwanza baada ya kuapishwa, Rais Samia Suluhu Hassan alionya kuhusu utaratibu uliokuwa ukitumiwa na serikali kuingia kwenye akaunti za wafanyabiashara na kuchukua pesa kwa kisingizo cha kukusanya kodi.

Aliitaka serikali kutafuta njia nzuri ya kukusanya kodi kutoka kwa wafanyabiashara bila kutumia nguvu kama vile kufungia akaunti zao.

Alisema hali hiyo imewatisha wafanyabiashara wengi ambao waliamua kuhamishia uwekezaji wao nchi zingine kutafuta mazingira rafiki ya biashara.

HABARI KITAIFA

## JK: Makaburu chanzo Kituo Polisi Selander

**Na Enock Charles**

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete amesimulia jinsi makaburu wa Afrika Kusini walivyosababisha kujengwa kwa Kituo cha Polisi Selander jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika kongamano la maadhimisho ya miaka 40 ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) jana mkoani Dar es Salaam, Kikwete alisema kituo hicho kilijengwa baada ya makomando wa makaburu kulilipua Daraja la Selander.

Alikumbusha kuwa kwenye eneo hilo jirani na daraja, palikuwa na hoteli ambayo baadaye walipewa polisi kutokana na hali ya usalama ya eneo hilo.

Kikwete alisema nchi zilizokuwa zikiunga mkono harakati za ukombozi ikiwamo Tanzania, ziliandamwa na vikwazo vingi kutoka kwa serikali ya makaburu wa Afrika Kusini.

"Pale Selander Bridge wazee wanakumbuka palilipuliwa mabomu, bahati nzuri tu lile daraja lilikuwa imara, lakini makomando wa Afrika Kusini waliingia, hatujui walifikaje.

"Kuna kitabu chao wameandika jinsi walivyosafiri wakaja kigamboni, wakaja pale wakategа mabomu lakini daraja halikulipuka na ndiyo siri ya kujengwa kituo cha polisi pale, hakikuwapo kabla," alisema.

## Bunge lataka kasi bima ya afya kwa wanajeshi

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, imeitaka serikali kuhakikisha awamu ya pili ya huduma za Bima ya Afya (Oktoba 2021 hadi 2026) inatekelezwe kama ilivyopangwa ili kuwezesha wanajeshi wengi kupata huduma za afya.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Vicent Mbogo, akiwasilisha maoni ya kamati hiyo wakati wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), alisema kuwa na bima kutawawezesha kutibiwa katika Hospitali za Jeshi, serikali, binafsi na mashirika ya dini.

Aidha, kamati hiyo iliitaka serikali kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya nyumba za makazi kwa wanajeshi itakayojumuisha nyumba 3,936 zilizobaki katika mradi wa nyumba 10,000 na kutenga bajeti ya utekelezaji wake ili kupunguza changamoto ya nyumba za makazi kwa wanajeshi.

Mbogo alisema pia ni muhimu serikali ikatoa fedha zote zilizotengwa katika mwaka 2020/2021 kwa ajili ya kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi.

"Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, hakuna fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli hiyo. Pamoja na nia njema ya serikali ya kutafuta mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya wanajeshi, Kamati inaishauri serikali kuhakikisha masharti ya mikopo hiyo yanaruhusu kuchagua mshauri elekezi na mkandarasi wa kujenga nyumba hizo ili kuhakikisha zinakuwa na viwango vya ubora unaotakiwa," alisema.




Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, akifungua Kongamano la Maadhimisho ya miaka 40 ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) lililofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwinyi alivyopotea Ulaya

**Na Enock Charles**

RAIS mstaafu wa awamu wa pili, Ali Hassan Mwinyi, amesimulia alivyopotea Uingereza na kulazimika kutembea umbali mrefu kuyatafuta makazi aliyofikia wakati akiwa mwanafunzi mjini Newcastle.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anasema siku hiyo alikuwa anarejea Newcastle kutoka London alikokwenda kwa ajili ya likizo ya chuo.

Anabainisha kuwa kipindi hicho alikuwa anaishi kwenye nyumba iliyokuwa inamilikiwa na Kanisa la Methodist, ikipokea wageni kutoka sehemu mbalimbali wakiwamo wanafunzi kutoka makoloni ya Uingereza.

Mwinyi anasema balaa lilianzia kituo cha treni alikokuwa kwenye foleni ndefu ya kukata tiketi pasi na kujua kwamba hakuwa na nauli kamili.

"Ilipofika zamu yangu nikatoa kiasi kilekile cha fedha kama nilizokatia tiketi wakati wa kuja London kutoka Newcastle, muuza tiketi akaniambia 'wewe husomi magazeti? Imetangazwa katika redio na kuandikwa magazetini kuwa nauli za treni zimepanda.

"Kusikia vile nikashtuka, nikatoa mfukoni mwangu pesa zote nilizokuwa nazo noti na sarafu nikamkabidhi, yule mzungu akaziangalia fedha zangu kwa dharau akachukua penseli aliyokuwa ameipachika kwenye sikio lake na kutumia ncha yake kuhesabia fedha nilizoweka mbele yake," anasimulia.

Anasema baada ya kuambiwa kuwa nauli yake haitoshi, aliamua kukata tiketi ya kuishia katika Mji wa Darlington badala ya Newcastle, ili baadaye maili 31 (Km 50) atatembea kwa miguu baada ya juhudi zake za kumshawishi mkatisha tiketi kumsamehe shilingi moja iliyokuwa imepelea kwenye nauli yake kugonga mwamba.

Hata hivyo, Mwinyi anasema alijitokeza mzungu aliyejitolea kumwongezea shilingi moja na hivyo kufanikiwa kusafiri hadi Newcastle kama alivyotarajia lakini anasema haukuwa mwisho wa matatizo yake kwa kuwa baada ya kufika huko Newcastle alipotea alipoamua kupita njia ya mkato badala ya kufuata barabara kubwa.

"Baada ya kuhangaika kwa muda, nikakutana na bwana mmoja nikamuuliza njia ya kunifikisha Methodisdt International House. Akaniambia tuongozane maana ya yeye anakwenda huko," anasimulia. Mwinyi anasema raia huyo mwema alimsindikiza hadi karibu na nyumba hiyo na kuhakikisha kuwa ameiona na yeye kurejea alipotoka jambo ambalo anasema aliliona ni la kiungwana na akabaini mzungu huyo hakuwa mkazi wa eneo hilo bali aliamua kumpeleka tu.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Access Microfinance Bank Tanzania Limited kupitia Kampuni za Madalali itauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Viwanja na Magari vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) tangu kutoka kwa tangazo hili, dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| NA. | TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | LUMUMBA | MASSAWE/SELESTINI GODFREY | TEGEREZEN/SULTAN NASSORO<br>MKEYENGE/S SUDI<br>ZILLINDE/BANABA GERALD | NYUMBA<br>NYUMBA<br>NYUMBA | MBAGALA-KIBURUGWE<br>MBAGALA-CHARAMBE<br>MBAGALA KIBURUGWE<br>DAR ES SALAAM | 10/6/2021<br>11/6/2021<br>12/6/2021.<br>SAA 4:00 ASUBUHI |
| 2. | LUMUMBA | CHALI/HUSSEN,CHALI | CHALI/HUSSEN,CHALI | NYUMBA | BUGURUNI-ILALA DAR ES SALAAM | 17/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 3. | LUMUMBA | MSECHU/PAUL,ALOYCE | MSHAMU/M,MWANAMOSI<br>MBAWALA/SIMON,JOHN<br>HUSSEIN/ABDUL,IDD | NYUMBA<br>NYUMBA<br>NYUMBA | MBAGALA-TEMEKE DAR ES SALAAM | 17/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 4. | LUMUMBA | BANI/RASHIDI,SAIDI | BANI/RASHIDI,SAIDI | ALTERNATIVE MORTGAGE NA NYUMBA YENYE HATI | | 17/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 5. | TEMEKE | ITEMBE/M,EMMANUEL | NDUKEKE/K.,SIMON | NYUMBA | TEMEKE | 18/6/2021 SAA 4: 00 ASUBUHI |
| 6 | LUMUMBA | KAMUGISHA/RICHARD, ANDREW | KAMUGISHA/RICHARD, ANDREW | ALTERNATIVE MORTGAGE NYUMBA | MBEZI KIBANDA CHA MKAA | 18/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 7 | TEMEKE | BILALI/SALEHE,ALLY | BILALI/SALEHE,ALLY | LESENI YA MAKAZI NA. TMK045715 | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | 18/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 8 | TEMEKE | SHABAANI,TATU | AKIDA/SAIDI,ALLIY | NYUMBA – ALTERNATIVE MORGAGE | TEMEKE | 18/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 9 | LUMUMBA | MREMA/JOHN,FRANCIS | MREMA/JOHN,FRANCIS<br>TAVERNA/RAFAEL, AGUSTINA<br>MSANGI/MUSSA,TERUZA | KUHAWILISHA-KIWANJA<br>NYUMBA- BOKO | KIGAMBONI<br>BOKO | 18/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 10 | LUMUMBA | MIREMO/MASIAGA,SULEYMAN | RWAMBO/ABDALLAH,SAID | NYUMBA | TEMEKE | 18/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 11 | LUMUMBA | JAFARAL/HUSSEIN,JOHA | MASELE/BONIPHACE, ADRIANO<br>BAKARI/A,BAKARI | NYUMBA | TEMEKE | 18/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 12 | PAMBA | ONDURU/GERALD, MAGRETH | ONDURU/GERALD, MAGRETH | NYUMBA HATI NA. 17424 | BUZURUGA - MWANZA | 4/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 13 | LUMUMBA | MPALALA/BAYONGA, HAWA | MASOUD/AHMED, MOHAMED | LESENI YA MAKAZI NA. TMK039912 | MBAGALA TEMEKE | 4/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 14 | LUMUMBA | MRISHO/BALTAZARY,RICHARD | MRISHO/BALTAZARY, RICHARD | NYUMBA YENYE HATI NA. 150343MG BLOCK N. PLOT NO.417 L.O 491747 | BAGAMOYO MJINI TOPTOP PWANI | 4/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 15 | LUMUMBA | MWAKISOLE/OBENI, MENGI | NJAWALE/COSMAS,MIRIAM | LESENI YA MAKAZI NA. TMK/MBK/MBK/25/177 | MBAGALA KUU TEMEKE- DAR ES SALAAM | 4/6/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA KUSHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED SIMU NAMBA. +255 677 860 000**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

## Makusanyo madeni ya matrekta yasuasua

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, limesema kuwa limekusanya zaidi ya Sh. milioni 465.1 kati ya Sh. bilioni 5.2 za matrekta na zana za kilimo kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, yaliyokopwa na watu mbalimbali wakiwamo watumishi wa umma.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2021/22, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, alisema fedha hizo ni madeni mbalimbali ambao kati yao ni watumishi wa umma.

Alisema mradi unaendelea na juhudi za ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wadaiwa sugu, ambao miongoni mwao walikuwa watumishi wa umma pamoja na watu binafsi.

"Shirika kupitia mradi wa matrekta limeendelea kuagiza na kuuza matrekta, vipuri na zana zake kwa bei nafuu ili kumfanya mkulima kuweza kumudu kununua," alisema.

Alisema maeneo tisa ya kipaumbele yatakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/22, huku akiidhinishiwa zaidi ya Sh. trilioni 2.35 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

Kwandikwa alibainisha maeneo hayo ni kuliimarisha jeshi kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa, mawasiliano, rasilimali watu pamoja na kutoa mafunzo kwa wanajeshi ili kuliongezea uwezo na weledi wa kiutendaji na utayari kivita.

Kingine ni kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi na nchi jirani, kuboresha mazingira ya kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma.

Pia kuendelea kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa zana na vifaa vya kilimo ili liweze kujitosheleza kwa chakula na kuboresha miundombinu katika vikosi ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi na kutoa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi.

Nyingine ni kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia, kuimarisha na kuratibu mafunzo ya Jeshi la Akiba na kuimarisha ushirikiano na jumuiya za kimataifa, kikanda na nchi moja moja katika nyanja za kijeshi na kiulinzi. Vilevile, kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia na kufanya upimaji, uthamini na ulipaji fidia ya ardhi katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya jeshi.

Alisema Wizara katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ili iweze kutekeleza majukumu yake inaomba iidhinishiwe na Bunge zaidi ya Sh. trilioni 2.35 kwa mafungu yote matatu.

Kati ya fedha hizo, zaidi ya Sh. trilioni 2.18 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na zaidi ya Sh. bilioni 176 ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo.



Baadhi ya Maofisa wa Jeshi la Wananchi (JWTZ) pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), wakiingia viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana, kuhudhuria uwasilishwaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 2021/2022. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wadaiwa sugu TBA kusakwa wiki ijayo

**Na Halfani Chusi**

WAKALA wa Majengo Tanzania (TBA) umewataka wadaiwa sugu walioko mkoani Dodoma kulipa madeni ya kodi wanayodaiwa kabla ya Mei 25, mwaka huu, yaani Jumanne ijayo, ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

Agizo hilo lilitolewa jana mkoani Dar es Salaam na Kaimu Mtendaji Mkuu wa TBA, Said Mndeme, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kuanza kwa mchakato wa kukusanya madeni kwa wadaiwa sugu mkoani Dodoma Mei 25, mwaka huu.

Alisema wadaiwa sugu walioko katika mkoa huo ambao ndiko yaliko Makao Makuu ya nchi, wakijumuisha taasisi na wizara ni zaidi ya Sh. bilioni moja.

Alisema kitendo cha baadhi ya wadaiwa kutolipa madeni kwa wakati kinakwamisha jitihada za TBA kuendeleza miradi mingine ambayo inategemea fedha kutoka kwa wadaiwa.

"Taasisi hii inahitaji fedha na fedha hizo mara nyingi zinatumika kwa ajili ya kukarababti na kuongeza nyumba, kuboresha makazi hasa kwenye nyumba za watumishi pamoja na kujenga nyumba mpya.

"Kwa hiyo, inapotokea taasisi au wizara hailipi kodi kwa wakati, maana yake wanakwamisha TBA kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha.

"Hii siyo kwa watumishi wa umma tu hata wale watumishi ambao wapo kwenye hizo nyumba lakini muda wao umekwisha kama vile wabunge ambao hawajafanikiwa kurejea tena bungeni, wanapaswa kuachia nyumba hizo kabla ya tarehe hiyo ili kupisha watumishi wapya kupata nyumba," alisema.

Aliongeza kuwa TBA wamefanikiwa kuwaondoa kwa nguvu wadaiwa sugu katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Lindi, Mtwara, Morogoro, Tanga, Iringa na Kilimanjaro na kuwataka Dodoma ambako mchakato unaelekezwa, kulipa kabla ya muda uliopangwa ili kuepuka usumbufu.

Sambamba na hilo, alisema kwa sasa wameboresha mfumo wa ulipaji kodi ambao mpangaji anaweza kulipia nyumba yake kwa njia ya simu ya kiganjani.

# Upinzani wajibu kauli ya CCM

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuwahimiza wanasiasa kufungua milango ya utengamano, maelewano na siasa zenye mashiko kwa mstakabali wa taifa, vyama vya upinzani vimesema suala hilo wamekuwa wakilipigia kelele kwa muda mrefu ingawa halikutekelezwa.

Juzi, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, alisema dhamira ya CCM bado ipo palepale kuhakikisha haishiriki siasa za mti kwa macho, piga nikupige au watu kuhasimiana kwa sababu za kisiasa.

Wakitoa maoni yao kwa nyakati tofauti jana, viongozi wa upinzani walisema milango ya upinzani ilikuwa wazi siku nyingi.

Ofisa Habari wa ACT- Wazalendo, Arodia Peter, alisema jambo hilo limekuwa likizungumzwa na upinzani muda mrefu na kuna wakati Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kiliwahi kusafiri kwenda Mwanza, kumwomba Rais aliyekuwapo wakati huo, Hayati John Magufuli, kuwe na mazungumzo na majadiliano.

Alisema ACT -Wazalendo nao wamekuwa wakizungumza namna nzuri ya kushirikiana na kuhakikisha nchi inakuwa kwenye mfumo mzuri wa demokrasia.

"CCM ndiyo iliua demokrasia ya Tanzania, walikuwa wanakandamiza uhuru wa watu kwa maana Tanzania ni nchi ya vyama vingi, lakini waliitoa kuwa ya chama kimoja.

"Waliwahi kusema watatufunga goli la mkono, maana yake ni uibaji wa kura wa waziwazi, kwa maana ya kuua demokrasia na kuwanyima watu uhuru wa kuchagua viongozi wanaowataka," alidai.

Alisema kama jambo hilo wameliona ni jema na wanataka wanasiasa kufungua milango, kwa upinzani ilikuwa wazi siku zote na kilio chao kilikuwa ni kuhakikisha nchi inakuwa huru na kujali demokrasia.

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa CUF, Mhandisi Mohamed Ngulangwa, alisema suala la kuwa na uwanja huru wa kufanya siasa siyo hiari ya CCM, bali katiba inaeleza na sheria inayoongoza kuhusu uwapo wa vyama vingi vya siasa inataka hivyo.

Alidai kuwa kilichokuwa kinafanywa mwaka 2016 mpaka mwaka 2020 kilikuwa ni ubabe na kukiuka sheria.

"Suala la kuhimiza wanasiasa kufungua milango ya utengamano na maelewano tunaweza kuitazama vizuri katika sura kwamba wanadalili ya kujirekebisha lakini upinzani hatuipokei kama hisani kwa sababu CCM haimiliki siasa za nchi hii.

"Nchi ilipoamua kuingia katika mfumo wa vyama vingi 1992 tuliamua tukiwa tunajua kwamba siasa za vyama vingi ni siasa zinazopelekea kuchagiza maendeleo na haikuwa hiari ya CCM kuamua lini waamue kuruhusu uwanja sawa na wakati gani wauminye."

Alisema kama wameamua kujirekebisha hiyo ni sifa njema, lakini hawapokei kama hisani kwa sababu huo ni wajibu Msajili wa Vyama vya Siasa, alitakiwa ausimamie katika muda wote wa uongozi wake.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema bado wanasubiri mazungumzo na Rais Samia Suluhu Hassan.

HABARI KITAIFA

# Nchemba aipongeza CRDB kutoa gawio kwa wanahisa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kuendelea kuwa kinara wa ubunifu wa huduma na bidhaa katika soko na kutengeneza faida kubwa inayoiwezesha benki hiyo kutoa gawio kwa wanahisa wake.

Dk. Nchemba alitoa pongezi hizo wakati wa semina ya Elimu ya Fedha na Uwekezaji iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wanahisa wake na Watanzania kuelekea Mkutano Mkuu wa Wanahisa unaotarajiwa kufanyika leo katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

Alisema Benki ya CRDB imekuwa ikishiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi kwa kusaidia miradi mbalimbali ya kimkakati inayotekelezwa na serikali, pamoja na kuwekeza katika kupanua wigo wa ufikishaji huduma na kuongeza ujumuishi wa kifedha kwa wananchi.

"Serikali inaichukulia benki hii kama kiongozi, na namna mnavyofanya vizuri inadhihirisha hilo. Nimesikia hapa mwaka jana mmetengeneza faida kubwa pamoja na changamoto ya COVID-19, hii inaonyesha uimara wa benki hii na uimara wa sekta ya fedha nchini kwetu, hongereni sana na asanteni kwa kutupa heshima," alisema na kuwahamasisha Watanzania kuwekeza katika hisa za benki hiyo ili kupata faida. Dk. Nchemba alisema ili sekta ya fedha iweze kufanya vizuri zaidi na uchumi wa Tanzania uendelee kukua kunahitajika elimu ya kutosha ya masuala ya fedha na uwekezaji kwa wananchi. Alisema kwa kutambua hilo mwaka 2011 serikali ilianzisha Mpango wa Taifa wa Elimu ya Fedha ikiwa na lengo la kujenga jamii yenye uelewa mpana wa masuala ya fedha, kuongeza ujumuishi wa kifedha na kuchochea ukuaji wa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa.

Pia alielezea mikakati inayowekwa na serikali kuboresha sekta ya fedha nchini kuwa wizara yake ina mpango wa kuandaa kikao kazi cha benki na wadau wengine wa sekta ya fedha ili kujadili changamoto zilizopo na maeneo ya uboreshwaji ili kufikia lengo. Akitaja baadhi ya mambo ambayo serikali imepanga kuyajadili, Dk. Mwigulu alisema ni pamoja na uboreshaji wa sera za usimamizi wa sekta ya fedha, upatikanaji wa mikopo kwa wafanyabiashara hususan wajasiriamali wadogo kwa kuhakikisha benki zinatoa mikopo yenye riba rafiki, kuongeza ajira kwa wananchi, kupanua wigo wa biashara katika nchi jirani na kuwajengea wafanyabiashara uwezo wa kushiriki katika biashara katika masoko ya kimataifa.

Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Ally Laay, alimshukuru Dk. Mwigulu kwa kuikaribisha benki hiyo kushirikiana na serikali katika kutekeleza mikakati ya kuimarisha sekta ya fedha nchini. Alimhakikishia kuwa benki hiyo itakwenda kuandaa sera ya kuelekeza na kusimamia uwezeshaji katika sekta mbalimbali za maendeleo nchini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema malengo ya semina hiyo ni kuwajengea uwezo wanahisa wao pamoja na Watanzania wengine ili kuwe na uwajibikaji wa kifedha na kuongeza ushiriki katika fursa za uwekezaji nchini pamoja na kupata uelewa wa huduma za benki hiyo zitakazowasidia kuboresha maisha yao.



Mafundi wakiongezea darasa moja katika shule ya sekondari Rusoli, Wilayani Musoma, mkoani Mara juzi. Shule hiyo ina madarasa 10 ambapo mahitaji ni madarasa 12. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wenye ulemavu walia ukosefu ajira migodini

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

MWENYEKITI wa Shirikisho la Chama cha Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Michael Nkanjiwa, amewaomba wamiliki wa migodi ya madini ya dhahabu kuwapatia ajira watu wenye ulemavu badala ya kuwabagua.

Nkanjiwa alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na Nipashe ilipotembelea kwenye ofisi za chama hicho wilayani Kahama.

Alisema Wilaya ya Kahama imezungukwa na migodi mingi ya uchimbaji madini ya dhahabu mikubwa na midogo, lakini cha ajabu watu wenye ulemavu hawapewi ajira kwa wingi hata zile nyepesi kwenye migodi hiyo.

"Tunaomba wamiliki wa migodi ya madini wilayani Kahama, wasitubague sisi watu wenye ulemavu, watupatie ajira zile ambazo tuna uwezo nazo kuzifanya kulingana na hali zetu, na wafuate sheria ya kuajiri walemavu asilimia tatu.

"Zipo kazi ambazo mtu mwenye ulemavu anaweza kuzifanya kwenye hiyo migodi, ikiwamo kufanya usafi, kutunza mazingira na hata kupanda miti," alisema.

Meneja wa mgodi mdogo wa machimbo ya dhahabu Ntambalale ulioko wilayani Kahama, Emmanuel Masanja, alisema kwenye mgodi huo hakuna mtu mwenye ulemavu ambaye ameajiriwa na hiyo inatokana na ugumu wa kazi zao.

Katibu Mkuu wa Mgodi wa Kasi Mpya ulioko Mwanzimba wilayani huko, Hosea Mbusule, alisema wameajiri watu wenye ulemavu wawili, ambao huwa wanafanya kazi za usafi na utunzaji wa mazingira.

## Sababu ya msururu wa meli bandarini Dar yatajwa

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), imesema kukua kwa mahitaji na biashara Bandari ya Dar es Salaam, husababisha msururu wa meli zilizo katika foleni kuhitaji huduma mahali hapo.

Imesema ili kukabiliana na hali hiyo, shirika hushirikiana na wadau kupunguza tatizo hilo, ikiwamo mawakala binafsi.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Meli kutoka TASAC, Nelson Mlali, amesema mzizi wa tatizo kubwa ni kuwapo gati chache ikilinganishwa na idadi ya meli zinazowasili nchini.

Mlali aliwaambia waandishi wa habari juzi, kwamba kila mwezi Bandari ya Dar es Salaam, inahudumia jumla ya meli 37.

Alisema aina ya mizigo inayopakuliwa na namna magati hayo yalivyotengwa ni ya bidhaa za chakula, mafuta ya kula, ya ndege, bidhaa zinazooza na zisizooza. Mlali alitaja vigezo vingine vinavyochangia foleni hiyo ni kutokana na kuwapo mizigo inayofanana, hali inayofanya meli husika ziwe katika foleni kwa sababu ya kutumia gati moja, hali iliyochangia hata foleni ya meli 10 za sasa.

Kuhusu namna bandari inavyojipanga katika ufanisi wa huduma zake, Mlali alisema kipaumbele hutolewa cha kupakua shehena zinazowasili bandarini, iwapo kuna msururu wa meli, huwa kwa bidhaa muhimu zenye hitaji kubwa wakati husika.

"Mfano unakuta kuna meli zimeingiza shehena aina mbili zote ni za mafuta. Lakini moja ni mafuta ya kula na nyingine ya ndege. Utakuta unaambiwa mafuta ya ndege yasiposhushwa leo, kesho 'airport' ndege haziruki.

"Sasa utaangalia kipi kianze, kwamba kesho kusiwe na 'flights', au uanze na mafuta ya kula, kipaumbele huwepo kwa kuangalia vitu vingi," alisema Mlali.

Alibainisha kwamba, tangu Februari mwaka jana hadi Aprili mwaka huu, limehudumia meli 439 zilizowasili nchini na kwamba hivi sasa kuna ongezeko la mahitaji ya huduma linalokua kwa asilimia 8.3.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Macho, masikio ya wadau wa soka nchini kwa Simba

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ya jijini Dar es Salaam wanatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kuwakaribisha wapinzani wao, Kaizer Chiefs kutoka nchini Afrika Kusini.

Mechi hiyo ni ya marudiano ya hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), na imepangwa kufanyika kuanzia saa 10:00 jioni kwa saa za hapa nyumbani.

Simba ambao ni vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, huku akiwa na mechi za viporo mkononi, watashuka katika mchezo huo wakiwa na kumbukumbu mbaya ya kichapo cha mabao 4-0 walichokipata kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa wiki iliyopita jijini Johannesburg.

Ili Simba iweze kusonga mbele katika mashindano hayo ya juu kwa ngazi ya klabu barani Afrika, inahitaji ushindi wa kuanzia mabao 5-0.

Katika mpira hakuna kisichowezekana endapo wawakilishi hao wa nchi watajiimarisha na wataongeza utulivu kwenye mechi hiyo itakayochezeshwa na mwamuzi, Pacifique Ndabihawenimana akisaidiwa na Emery Niyongabo na Pascal Ndimunzigo, wote kutoka Burundi.

Kama Kaizer Chiefs iliweza kupata ushindi huo mnono ilipocheza nyumbani kwake, hali kadhalika Simba inayofundishwa na Mfaransa Didier Gomes na msaidizi wake, Selemani Matola ina uwezo wa kulipiza kisasi au 'kupindua' meza kama wadau wa soka wanavyopenda kusema.

Wachezaji wa Simba wanatakiwa kila mmoja anatakiwa kutimiza vyema majukumu yake katika mchezo huo ambao utafuatiliwa na mashabiki wengi wa soka barani Afrika hasa kufuatia Mnyama kuwa na rekodi nzuri anapocheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Endapo kila mchezaji atacheza kwa kiwango cha juu, ni wazi Simba itaweza kulipiza kisasi na hatimaye kusonga mbele kwenye michuano hiyo huku ikivunja rekodi nyingine ya muda mrefu ambayo iliwahi kuiweka katika michuano hiyo ya kimataifa.

Kama Simba iliwahi kufungwa mabao 4-0 hapa nyumbani na katika mchezo wa marudiano ugenini ilifanikiwa kuwachapa Mufurila Wanderers magoli 5-0, Nipashe inaamini hakuna kitakachoshindikana kwa Wekundu wa Msimbazi kupata ushindi wa aina hiyo na kuendelea katika michuano hiyo.

Tunawakumbusha wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa Simba kila mmoja kutekeleza majukumu yake kwa asilimia 100 ili kufikia malengo ambayo waliyatarajia kufikia kwenye michuano ya mwaka huu baada ya kupata matokeo bora zaidi kwenye hatua ya makundi.

Kama Simba iliweza kupata ushindi mnono dhidi ya mabingwa wa Sudan, El Merreikh na vile vile kuwafunga mechi zote mbili (ugenini na nyumbani), dhidi ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), basi inawezekana pia kufanya miujiza ya kuwafunga na kuwaondoa wajukuu hao wa Mandela na kuitikisa Afrika kwa mara nyingine.

Kama kulikuwa na wakati muhimu kwa mashabiki kuishangilia timu yao, huu ndio ule muda muafaka wa mashabiki kutimiza jukumu lao la ushangiliaji kuanzia dakika ya kwanza hadi ya mwisho ya mchezo, ushangiliaji wenye mwembwe na usio wa kusitasita, utawaongezea morali wachezaji na kupata nguvu zaidi ya kupambana katika mchezo huo.


Imani ambayo ilikuwapo kwa timu katika mechi za makundi, inatakiwa kuendelea katika mchezo huu wa leo ambao Simba ikisonga mbele, matokeo yake yatawekwa kwenye kitabu cha kumbukumbu.

Nipashe inaamini hakuna kisichowezekana endapo wachezaji wa Simba watacheza katika kiwango chao kilichozoeleka na kwa mara nyingine kumwenzi aliyekuwa Rais, marehemu, Dk. John Pombe Magufuli kwa klabu ya Tanzania kubeba Kombe la Afrika.

Mungu ibariki Simba, Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mvunja kwao hakui ila...

"MVUNJA" kwao hakui ila huwa yeye mbombwe (bombwe.) 'Bombwe' ni funza, buu au gae la chungu. Pia ni kitu duni. Maana yake anayeivunja au kuisaliti nchi yake hakui au hana thamani, hubakia mtu wa kudharauliwa. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu anayeisaliti nchi yake. Vilevile hutumiwa kutufunza umuhimu wa kuzipenda nchi zetu.

Leo Jumamosi timu ya Simba itacheza mechi ya marudiano dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mchezo wa kwanza ulifanyika kwenye Uwanja wa FNB jijini Johannesburg, Afrika Kusini zilikopambana Simba na wenyeji Kaizer Chiefs, kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ilifungwa mabao 4-0.

Kipigo hicho kilisababisha Ofisa Habari wa Klabu ya Simba, Haji Manara azimie mara mbili kwenye hoteli aliyofikia akisema hali yake ilikuwa mbaya sana. Akasema alikuwa na presha, yaani shinikizo la damu. Aliweka bayana kuwa mchezo wa mpira kuna siku unaweza kutwaa uhai wake!

Namshauri Manara awache/aache kwenda viwanjani wakati timu yake inapocheza na zingine kwani anaweza kuanguka na kupoteza maisha ilhali bado yu kijana kwa kile kisemwacho "fuo bado" yaani mtu mwenye umri wa baina ya utoto na makamo. Kuna watu kadhaa waliopoteza uhai wakati Simba na Yanga zinapopambana, hasa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Wakati Simba ikipambana na Kaizer Chiefs leo jioni nawashauri watu wasiopenda au wasioitakia heri/kheri (hali ya ufanisi) timu yetu ya nyumbani, Simba, kutokwenda uwanjani. Kwa kufanya hivyo tutaficha chuki baina yetu, yaani Simba na Yanga zilizo mtaa, mkoa na nchi moja- Tanzania!

Wahenga walisema: "Chuki humchoma anayeihifadhi." Kwa kawaida chuki humsumbua anayeiweka au kuihifadhi. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutoiweka chuki kwa kuwa tunajidharau wenyewe. Ni dhahiri kuwa 'Chuki' ni hisia ya kutopenda kitu au jambo. Kama ndivyo kwa nini Simba na Yanga ziwekeane chuki?

Kama ni lazima wababe hao wa Tanzania wafanyiane chuki wao kwa wao nchi ni lazima lakini zinapocheza na timu ngeni za n-nje ya Tanzania watupilie mbali chuki zao.

"Ni lipi lisilo nduguye na mwamu wake? Maana yake ni jambo au tukio lipi ambalo halina linalohusiana nalo au jenzake (ndugu au mwamu?) Methali hii hutumiwa kumkumbusha mtu kwamba awafanyiapo wenzake mabaya lazima hata naye ataishia kufanyiwa mabaya. Tuwafanyiayo wenzetu watatufanyia hayo sisi.

"Nasihi" ni kitendo cha kumshauri mtu na kumwelekeza afanye mambo mema; sihi. Kitendo cha kumsemesha mtu kwa upole na kwa maneno mazuri ili aridhie jambo analoambiwa.

Kwa hiyo nawasihi Yanga wajaze maeneo yao ya kukaa kwenye Uwanja wa Mkapa leo wakiwa wamevaa mashati ya njano na kijani na bendera zao mikononi na kuishangilia Simba mwanzo mwisho itakapokuwa inapambana na wapinzani wao kutoka Afrika Kusini. Jambo hilo laweza kuwashangaza na kuwashtua Kaizer Chief.

Endapo itakuwa hivyo, huenda ushangiliaji wao (Yanga) ukawafanya wachezaji wa Simba kupata nguvu na mori zaidi, na kushinda mechi hii ya nyumbani huku wageni kutoka Afrika Kusini wakibaki kushangaa kutokana na mashambulizi ya Simba yatakayoinyang'anya Kaizer Chiefs tonge mdomoni.

Wahenga walisema: "Mtu hauzi kabila lake." Maana yake mtu haliuzi kabila lake au watu wake. Methali hii hutumiwa kutukumbusha umuhimu wa kuzionea fahari asili au nchi zetu. Twakumbushwa kuwa lazima tuwe na uzalendo yaani hali ya mtu kuwa na nasaba ya asili ya nchi; hali ya mtu kujitolea kwa hali na mali kwa ajili ya nchi yake.

Bila shaka kuna watakaosema mimi ni shabiki wa Simba, HAPANA. Mimi ni mwanachama wa Yanga tangu tarehe 2/12/1966 nikiwa na kadi namba 447 mbali ya kadi zingine tatu za mwaka 1976, yenye namba 01868 na namba 0340 ya mwaka 1993 nitaendelea kuwa mwanachama mpaka siku ya mwisho.

Kwa Yanga na Simba, hasa mashabiki, nawaambia: " Mwenye busara mara hunasihika." Maana yake mtu mwenye hekima huufuata ushauri apewapo. Hutumiwa kutukumbusha umuhimu na faida za kuyafuata mashauri tupewayo na wazazi wetu au watu wanaotuzidi maarifa.

Wahenga walisema: "Mwekaji kisasi haambiwi mwerevu." Maana yake anayemwekea mwenzake kisasi hawezi kusemekana kuwa ni mwerevu kwa kufanya hivyo. Methali hii inatukanya na kutunasihi tusiwe na tabia ya kuwekeana kisasi au kuwa na kinyongo na watu wengine.

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

HABARI PICHANI

# RAIS WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA WATU NA HAKI ZA BINADAMU ATEMBELEA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (wa pili kushoto) akitoa maelezo kwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Watu na Haki za Binadamu (ACHPR), Jaji Sylvain Ore (wa pili kulia) na ujumbe wake, walipotembelea ofisi za kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni Viwandani, mkoani Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga.



Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (kulia), akifafanua jambo kwa Jaji Sylvain Ore, alipotembelea kiwanda hicho.




Mratibu wa vipindi wa EATV, Sophia Mnganya (kushoto), akitoa maelezo kwa wageni.



Mhariri wa Michezo Radio One, Amri Massare (kushoto), akitoa maelezo kwa wageni waliotembelea studio za redio hiyo.



Mkurugenzi wa Vipindi vya Televisheni ya ITV, Pius Paul (kulia), akitoa maelezo kwa wageni waliotembelea ofisi hizo.



Mkuu wa Idara ya Habari wa ITV, Steven Chuwa, akitoa maelezo kwa wageni waliotembelea ofisi za ITV Mikocheni, jana. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**

# Serikali yatoa kauli kuhusu ulipaji malimbikizo madeni ya w'biashara

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa ni lazima Wizara ya Fedha na Mipango ipime athari na faida katika kufuta madeni ya wafanyabiashara wa ndani yaliyolimbikizwa kwa miaka ya nyuma.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hamad Yussuf Masauni, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbogwe(CCM), Henry Maganga.

Katika swali lake, Mbunge huyo aliyehoji kuhusu mpango wa serikali kuwafutia wafanyabiashara wa ndani madeni ya nyuma.

"Serikali ina mpango gani wa kufuta madeni ya muda mrefu kwa wafanyabiashara wa ndani yatokanayo na ukosefu wa elimu juu ya matumizi sahihi ya mashine za EFD wanayodaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Masauni alisema mwaka wa fedha 2018/19, serikali ilitoa msamaha kwa wadaiwa wa kodi ili kuongeza makusanyo.

Alisema msamaha huo ulihusisha riba na adhabu zinazoambatana na madeni yote yaliyolimbikizwa kwa miaka ya nyuma.

Hata hivyo, alisema msamaha huo ulilenga kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba na adhabu kwa kiwango cha asilimia 100 kwa wafanyabiashara wote hapa nchini ambao walikuwa na malimbikizo ya madeni ya kodi.

"Msamaha huu ulitolewa kwa kipindi cha miezi sita kilichoanzia Julai 1, 2018 mpaka Desemba 31, 2018 ambapo kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wake, serikali iliongeza muda wa msamaha huo kwa miezi sita ili wafanyabiashara waliokuwa na madeni hayo kuweza kukamilisha malipo husika yaliyotokana na msamaha huo," alisema.

Aidha, alisema hatua hiyo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 ilitarajiwa kuongeza mapato ya serikali na kukusanya malimbikizo ya madeni ya nyuma ya kodi pamoja na kuinua kiwango cha ulipaji kodi kwa hiari kwa zaidi ya asilimia 10.

Alisema licha ya nia nzuri ya serikali ya kufuta riba na adhabu ili kuwawezesha walipakodi wenye madeni sugu ya kodi kuyalipa kwa awamu ili kurahisisha mwendelezo wa biashara zao.

"Wengi wao hawakulipa kodi hizo hata baada ya kuingia mikataba na TRA na hata baada ya Serikali kuongeza muda wa ziada wa kufanya malipo ya kodi husika yaliyotokana na msamaha huo," alisema.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, akijibu swali Bungeni kuhusu msamaha kwa wadaiwa wa kodi jijini Dodoma. **PICHA: WFM**

# Ujenzi wa meli mpya watengewa bil. 135/-

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL,) imetenga Sh. bilioni 135 kwa mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya kutekeleza miradi tisa ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria na Tanganyika.

Aidha, imesema taratibu za kusaini mkataba wa ukarabati wa Meli ya MV Liemba unakamilishwa na utasainiwa mwanzoni wa mwezi Juni, mwaka huu ili kazi ianze.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliitoa kauli hiyo bungeni jana wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Irene Ndyamukama.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji lini serikali itakarabati meli ya MV Liemba pamoja na kujenga meli mpya ambazo zitachochea ukuaji wa uchumi Mkoa wa Rukwa. Waitara akijibu swali hilo, alisema pamoja na kutekeleza mradi wa ukarabati wa meli ya MV.Liemba katika Ziwa Tanganyika, serikali pia imepanga kutekeleza miradi ya ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika.

Alisema ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo katika Ziwa Tanganyika na ukarabati mkubwa wa meli ya kubeba shehena ya mafuta ya MT, Sangara katika Ziwa Tanganyika.

Alisema mikataba ya miradi hiyo ipo katika hatua za mwisho kusainiwa mapema mwanzoni mwa mwezi Juni, 2021.

"Ni matumani yangu kuwa, kukamilika kwa miradi hii kutaondoa adha ya usafiri kwa njia ya maji katika Ziwa Tanganyika na mikoa jirani na Kigoma," alisema.

Alisisitiza hatua hiyo itaimarisha na kuifanya nchi kuwa kiungo kikubwa cha soko pana la pamoja linalokisiwa kuwa na idadi ya watu takribani milioni 10 wanaoishi pembezoni mwa ziwa hilo katika nchi za Mashariki na Kati ya Afrika ikijumuisha nchi za Tanzania, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo aliyehoji ni lini ukarabati wake utaanza kwa kuwa meli hiyo imedumu miaka 100.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Waitara alikiri meli hiyo ni ya siku nyingi na kuahidi kuwa kwa kuwa zabuni ilishatangazwa na mkandarasi wa ujenzi kupatikana mwezi ujao mkataba utasainiwa ili kazi ianze.

# Ataka mkakati kuwaondolea mzigo wanawake

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira, ameitaka serikali kuweka mkakati wa kuwakomboa wanawake wanaobebeshwa mzigo mkubwa wa kugharamia matunzo ya watoto bila msaada wa baba.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanahamis Ali Khamis, akijibu swali la Mbunge huyo, alitoa rai kwa wananchi wote kutambua kuwa jukumu la kutunza familia ni la wazazi wote wawili na asitokee mmojawapo kutegea kwa kutotoa matumizi.

Alisema serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wanaotoa wanawake tangu enzi za kupigania uhuru na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Naibu Waziri huyo, alisema katika kuwakomboa wanawake hao wanaobebeshwa mimba na kuachwa bila matunzo, serikali imeandaa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 ambayo pamoja na masuala mengine inatoa maelezo kuhusu matunzo kwa mtoto kutoka kwa wazazi wote wawili.

Alisema Sheria hiyo kupitia kifungu cha 7(1), kifungu cha 8(1) a – g, kifungu cha 8(2) na Kifungu cha 9(3) a na b imetoa maelezo kwa wazazi kuhakikisha kuwa mtoto anapata matunzo yote stahiki ili kuhakikisha kuwa haki na ustawi wake vinatimizwa.

"Sheria hii pia kupitia kifungu cha 44 (a – e) na Kifungu cha 45(1) pia imetoa maelezo endapo wazazi wa mtoto kama hawaishi pamoja na kama mtoto atakuwa anaishi na mzazi wake wa kike yaani mama, basi mzazi wa kiume atawajibika katika kugharamia malezi ya mtoto wake kulingana na kipato alichonacho na mazingira anayoishi mtoto husika," alisema.

Aidha, alisema sheria hiyo pamoja na kanuni zake imekuwa ni msaada mkubwa katika kuhakikisha kuwa mzigo wa kugharamia malezi ya watoto unawagusa wazazi wa pande zote mbili yaani baba na mama wa mtoto.

**"Sheria hii pia kupitia kifungu cha 44 (a – e) na Kifungu cha 45(1) pia imetoa maelezo endapo wazazi wa mtoto kama hawaishi pamoja na kama mtoto atakuwa anaishi na mzazi wake wa kike yaani mama, basi mzazi wa kiume atawajibika katika kugharamia malezi ya mtoto wake kulingana na kipato alichonacho na mazingira anayoishi mtoto husika," alisema.**





# Viwanda vya kuzalisha dawa za binadamu vyapewa somo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limevitaka viwanda vinavyozalisha dawa za binadamu kuhakikisha kidonge kimoja hakizidi wala kupungua uzito ili kulinda afya ya watumiaji.

Akizungumza juzi kwenye maadhimisho ya siku ya vipimo duniani, Mkurugenzi wa Upimaji na Metrolojia kutoka TBS, Mhandisi Johanes Maganga, alisema vipimo vinaathiri afya hivyo ni muhimu viwanda kuzingatia hilo.

"Mfano unapoenda dukani kununua panadol mbili kwa ajili ya maumivu ya kichwa dawa hizi zinapaswa kuwa katika uzito wa miligramu 500 kwa kila kidonge."

"Viwanda vinavyozalisha vinapaswa kuhakikisha kidonge kimoja hakizidi wala kupungua uzito ili kulinda afya ya watumiaji na ukienda kununua na ukikuta mtengenezaji ametengeneza chini ya hapo akakupa chini ya miligramu 450 ina maana ukikinunua inawezekana kisiende kutibu ule ugonjwa," alisema.

Mhandisi Maganga alisema huduma bora za afya zinawezekana kwa kuzingatia ubora wa vipimo unaotolewa na TBS.

Akifungua maadhimisho hayo, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Magonjwa yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. James Kiologwe, aliitaka TBS kutoa elimu kwa wananchi ili kutambua vipimo sahihi ni vipi na wapi wapate hivyo vipimo sahihi.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Abel Makubi, alisema: "Nitoe wito kwa TBS kutoa elimu kwa wananchi kuweza kutambua vipimo sahihi ni vipi na wapi wapate hivyo vipimo sahihi. Tunafurahi kwamba taasisi zimezungumza ninyi ni walinzi wa Taifa mnaweka viwango vya ubora lakini pia mnasimamia hivi viwango na si viwango tu hata wazalishaji nao pia mnawasimamia." Alisema wizara ina wajibu wa kuonyesha kwamba sera, sheria, kanuni na taratibu zinafuatwa katika masuala ya vipimo kwa kuhakikisha mtoa huduma na elimu na ujuzi pamoja na maarifa ya kutosha kuhusina na kupima.

"Swali lingine ambalo tunapaswa kujiuliza ni hivi vifaa tunavyovitumia ni sahihi ni wajibu wa sisi wenye mamlaka kusimamia pamoja na kuhakikisha wanaotoa huduma na vifaa vyao vinaruhusu kufanya vipimo," alisema.

Aliongeza: "Ni muhimu kujua nani anafanya hiyo huduma nimefurahishwa sana na taarifa ya mkuu wa chuo kwamba wanataka kujenga maabara ya kisasa nami nawapongeza sana."



Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi (kushoto), akipokea zawadi yenye picha yake aliyopigwa wakati akila kiapo cha Maadili ya Utumishi wa Umma kutoka kwa Watumishi wa Ofisi yake Binafsi, Lilyberthmark Mrema (katikati) na Bertha Majili (kulia), katika Ofisi ya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Mgogoro wa ardhi wa miaka 33 watatuliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MGOGORO wa ardhi uliodumu kwa takriban miaka 33, baina ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma na wakazi wa Mtaa wa Ndachi Kata ya Mnadani, umepatiwa ufumbuzi baada ya pande hizo kufikia makubaliano ya kuruhusu kazi za upimaji na urasimishaji makazi kuendelea.

Akizungumza jana na wananchi, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, alisema kuwa baada ya kumalizika kwa mgogoro huo wataanza mara moja kazi ya ugawaji viwanja pamoja na kushughulikia kero zilizopo kwa haraka.

"Wananchi wa Ndachi mlijicheleweshea wenyewe maendeleo kutokana na migogoro hii ya ardhi basi niwaombe kutokana na makubaliano ya leo sasa mtupe nafasi tuanze kazi ya kugawa viwanja na upimaji ili tumalize kama ambavyo tumefanya katika maeneo mengine," alisema Mafuru.

Alisema gharama za upimaji kwa mwananchi ambaye amekutwa katika eneo na kufanyiwa urasimishaji itakuwa ni Sh. 150,000 na kwa wenye viwanja vingi watachukua asilimia 70 ya maeneo yao na jiji litachukua asilimia 30. Alieleza asilimia 30, inayochukuliwa na Jiji itatumika kwa ajili ya kufidia viwanja kwa wale ambao watapitiwa na miundombinu mbalimbali kama vile shule, hospitali pamoja na barabara.

Hata hivyo, alisema kuwa katika kukamilisha kazi hiyo watakuwa wanahudumia wakazi 100 kwa awamu hadi watakapo wafikia wote na kukamilisha mradi huo wa upimaji na urasimishaji wa makazi.

Naye Diwani wa Kata ya Mnadan, Paul Bankiye, alisema kuwa mgogoro huo umedumu kwa takribani miaka 33, umechangia kwa kiasi kikubwa kurudisha nyuma maendeleo ya mtaa huo.

Alisema kuwa sababu kubwa za mgogoro huo ilikuwa ni kutoafikiana na uongozi wa Jiji katika mikataba ya upimaji ardhi pamoja na urasimishaji wa makazi.

"Leo mkurugenzi wa jiji amefika katika mtaa wetu na timu ya viongozi wa jiji la Dodoma akiwemo Naibu Meya na kutoa ufafanizi ambao kila mtu ameridhika na tunachosubiri sasa ni kuanza shughuli ya upimaji na ugawaji wa viwanja," alisema Bankiye.

Aidha alisema kuwa wameamua kufikia muafaka kutokana na uongozi wa jiji kuyazingatia yale ambayo wananchi walikuwa wanayapendekeza ambayo ndiyo yalikwamisha zoezi la upimaji kwa muda mrefu.

Alishukuru Jiji kwa kufanya kile ambacho wananchi walikuwa wakikilalamikia siku zote na kuzua migogoro isiyokuwa na tija.

"Sasa zoezi la upimaji, ugawaji wa viwanja pamoja na urasimishaji wa makazi litaendelea hivyo niwaombe wananchi kutoa ushirikano katika kanuni zoezi hili ili liende kwa kasi," alisema Bankiye.

Vile vile, aliwataka wananchi kuwa makini na matapeli kwani kutokana na kuanza rasmi kwa kazi ya ugawaji viwanja watatumia fursa hiyo kutaka kufanya utapeli.

# Askofu ayakubali mapendekezo ya kamati ya corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Makanisa ya Free Pentecostal Church Tanzania (FPCT), Stevie Mulenga, ameunga mkono mapendekezo ya wataalamu wa kamati iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan juu ya utoaji wa chanjo ya ugonjwa wa corona.

Kutokana na mapendekezo hayo, amewatoa hofu Watanzania kuhusu uamuzi utakaotolewa na serikali kuhusu chanjo.

Askofu Mulenga, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa semina elekezi ya viongozi wa kanisa hilo jimbo la Dodoma iliyofanyika katika Kanisa la FPCT Nkuhungu.

Katika semina hiyo ambayo mada kuu zilikuwa ni uadilifu, uaminifu, uwajibikani na uwajibishwaji.

Alisema yeye hana mashaka na chanjo ambayo wataalamu wa afya wameshauri itumike lakini anayo imani kubwa kuwa Watanzania watakiwa kuendelea kumtegemea Mungu.

"Kufa kupo palepale hata kama utachanja kama Mungu amepanga kinachotakiwa pamoja na chanjo hii tumtangulize Mungu kama ambavyo Hayari Rais John Magufuli alivyokuwa ametujengea imani kubwa juu ya ugonjwa huu ili tuondokane na hofu," alisema Askofu Mulenga.

Alisema anaunga mkono pia mapendekezo ya kamati hiyo maalum ambayo inapendekeza utoaji wa chanjo hiyo uwe wa hiari na siyo kulazimisha watu.

"Mimi sina shaka na chanjo kwani hata nikiwa mdogo nilichanjwa chanjo ya ndui lakini ninachotaka kuwaambia Watanzania ni kwamba waondokane na hofu juu ya ugonjwa huu na kuuogopa kuliko hata tunavyo mwogopa Mungu," alisema askofu huyo.

Kuhusu uadilifu na uaminifu, alisema kuwa njia pekee ya taifa na kanisa kuwa na maendeleo ni lazima kuzingatia misingi hiyo.

"Ili kuwa na taifa imara na uchumi imara ni lazima kuwa na viongozi wenye sifa za uadilifu na uaminifu ambao hawatafanya mambo kwa ajili ya matumbo yao binafsi," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi wa dini kufanya mambo ambayo ni utaratibu wa misingi ya dini na kuacha kufanya vitu ambavyo vitawafanya watu wengine kuwa na shaka nao.

"Kumekuwapo na tabia ya viongozi wa dini kutembea na katoni za maji pamoja na chumvi wakiuza kwa waumini kwa madai kuwa wakitumia maji hayo au chumvi ile basi watapata mafanikio.

"Kama wanataka kuwa viongozi wa dini waendele na dini na kama wanataka kuwa wafanyabiashara wafuate utaratibu ilikiwa ni pamoja na kupata leseni kwani wanauza maji bila hata kutoa risiti huo ni wizi wa mapato ya serikali," alisema.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud (wa pili kushoto), akiifariji familia ya Mbunge wa Jimbo la Konde, marehemu Kharib Said Haji, baada ya kuhudhuria maziko yake huko Kisiwani Pemba juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yafarijika utatuzi kero za Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imefarajika na mafanikio ya vikao vya sekretarieti ya kitaifa ya kujadili hoja na changamoto za Muungano, ambapo hoja nane zinatarajiwa kutatuliwa katika kipindi kifupi.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, alipofanya mazungumzo na sekretarieti ya kitaifa inayojadili changamoto za Muungano ofisini kwake kwa ajili ya kujitambulisha.

Abdulla alisema ushirikiano mzuri uliopo kati ya ofisi yake na ofisi ya Makamu wa Rais unatokana na maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungamo, Samia Suluhu Hassan, uliowapa watendaji hao chini ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dk. Philip Mpango. Aidha, alipongeza ushirikiano mzuri uliopo kati ya ofisi yake na Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kwa kufanya kazi kwa karibu na matokeo yake yamesaidia kuwa kiungo kikuu cha ushirikiano na kufanikisha malengo hayo.

Abdulla aliwaambia wajumbe hao kwamba serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, imesisitiza na kuweka kipaumbele cha kutatuliwa kwa changamoto hizo kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla.

"Nimefurahishwa na ujio wenu katika kikao hiki cha kwanza, ambapo malengo ni kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto za Muungano kama viongozi wetu wakuu wanavyotaka kuona suala hili linafikia mwisho wake," alisema.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Merry Maganga na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Tixon Mzonda, waliahidi sekretarieti kuzifanyia kazi changamoto zote ziliopo.

Maganga alisema sekretarieti hiyo imeundwa likiwa ni agizo la Rais Samia, ambapo wametakiwa kuzipatia ufumbuzi changamoto ziliopo katika Muungano.

"Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, tumefurahi kukuona na tunaomba ushirikiano wako zaidi tutakapopata vikwazo katika utekelezaji wa kazi za sekretarieti hii," alisema.

# Wakulima washauriwa kilimo cha viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA wametakiwa kujikita zaidi katika kilimo cha mazao ya viungo, ambacho bei yake ni kubwa katika soko la dunia.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Dk. Soud Nahoda Hassan, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais, Anna Atanas Paul, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, aliyetaka kujua serikali imejipanga vipi kuwahamasisha wakulima kulima mazao ya viungo, ambayo soko lake ni kubwa la uhakika nchi za nje.

Dk. Hassan alisema ni kweli kwa mujibu wa taarifa za bei ya mazao katika soko la dunia, mazao ya viungo yanaongoza kwa bei nzuri yenye tija kwa wakulima kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Aliyataja mazao ya viungo ambayo bei yake ni nzuri katika soko la dunia ni vanila, pilipili manga, pilipili hoho, uzile na mdalasini.

"Mheshimiwa Spika, mazao haya ya viungo bei yake hivi sasa ni nzuri kwa mkulima, ambayo inaweza kumuinua na kupiga hatua kubwa ya maendeleo," alisema.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na wizara ya kilimo kwa sasa ni kutoa elimu na mbinu za kuimarisha kilimo hicho kwa kushirikiana na taasisi binafsi zinazofanya kazi za kilimo na maendeleo yake.

Alieleza kuwa kazi ya kutoa elimu kwa wakulima katika kuimarisha kilimo cha mazao ya viungo itatekelezwa na kusimamiwa na mabibi shamba na mabwana shamba wa Unguja na Pemba.

Alisema matarajio ya wizara ni kuona wakulima wanaitikia wito wa kilimo cha mazao ya viungo ambacho soko lake kubwa lipo katika nchi za la Asia Mashariki ya Kati, mashariki ya mbali na Ulaya.

"Mheshimiwa, hakuna sababu ya wakulima wetu washindwe kuyafikia mahitaji ya soko la mazao ya viungo, kwa sababu ardhi yetu ni nzuri inayokubali kwa mazao ya aina hiyo," alisema Hassan.

Alisema Zanzibar katika miaka ya 1960 ilikuwa maarufu kwa usafirishaji wa mazao ya viungo katika soko la la mashariki ya mbali yakiwamo mafuta ya nazi yanayotokana na malighafi ya mbata.

# Majengo ya magofu kufanyiwa ukarabati

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar inatarajia kuyafanyia ukarabati mkubwa majengo ya magofu ya kale yaliopo Mwinyimkuu Dunga Wilaya ya Kati na Mkamandume Pemba, kwa ajili ya kuitangaza sekta ya utalii Zanzibar.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Leila Mohamed Mussa, wakati akiwasilisha makadirio mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2012-2022 katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema matengenezo ya majengo hayo yatagharimu Sh. bilioni moja na kwamba serikali haiwezi kutegemea sekta ya utalii wa fukwe pekee, kwa kuwa utalii wa majengo ya makumbusho ya kale ni moja ya tegemeo ya sekta hiyo.

Alisema serikali imeshalipa fedha kwa mkandarasi Sh. 865,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa magofu ya Mkamandume Pemba.

Kwa upande wa ujenzi wa majengo ya kale ya Mwinyimkuu yaliopo Dunga, alisema, ujenzi umefikia asilimia 93, huku mkandarasi akilipwa fedha kwa ajili ya mradi huo.

Alisema majengo ya kale hayo yamebeba historia kubwa ya Zanzibar ambapo alitolea mfano kwa Mwinyimkuu yaliopo Dunga, kwamba yalikuwa ndiyo makao makuu ya mtawala wa kwanza wa kienyeji wa Zanzibar kabla ya kuja kwa utawala wa Sultani wa Oman.

Aidha, alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar imejipanga kuitangaza Zanzibar kwa kushiriki maonyesho mbalimbali ya kitalii yanayofanyika duniani kote.

Alisema maonyesho ya kitalii ya kimataifa ni moja ya fursa nzuri ya kuitangaza Zanzibar, ambayo huwawezesha watendaji wa kamisheni kuvitangaza vivutio viliopo Zanzibar na kufahamika.

"Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, serikali imekusudia kuimarisha majengo ya kale kwa ajili ya kuimarisha utalii wa kihistoria, ambapo pia Zanzibar imejipanga vizuri kushiriki maonyesho yote ya kimataifa yatakayofanyika katika mabara yote ili kutangaza vivutio viliopo," alisema.

Alieleza kwamba serikali ya Oman imeahidi kuendelea na ukarabati wa jengo lililoporomoka la Beit-al-jaib mwishoni mwaka jana.

Alisema ukarabati wa jengo hilo unaendelea katika hatua ya awali ya uchunguzi wa udogo kujua uwezo wake kwa mujibu wa ushauri wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), ambalo ndilo linaloshughulikia majengo ya kale yaliopo chini ya urithi wa kimataifa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**BURNA BOY, ULIPOFIKA TEMA MATE CHINI** Uk.14

JUMAMOSI MEI 22, 2021



## UJUMBE KWA SADALA

# Kiba atumia fumbo kumnanga mtu

NI ujumbe uliowafanya mashabiki na wapenzi wa burudani kuwa njia panda kujua ni nani hasa Staa wa Bongo Fleva nchini, Ali Kiba, amemlenga.

Hata hivyo, jina la Sadala alilotumia msanii huyo limesababisha mjadala mkubwa kutokana na kila mtu kutoa maana tofauti.

Katika ujumbe wake kupitia ukurasa wa Twitter, Kima amemsihi Sadala kuacha kulalama kwa kuambiwa hana pesa, kwani Watanzania wakiamini yeye ni tajiri inatosha.

Ikumbukwe hivi karibuni, mwanamuziki nyota Afrika Mashariki, Diamond Platnumz, alikasirishwa na hatua ya jarida la Fobes, kutoa orodha ya wasanii matajiri barani Afrika, huku jina lake likiwa la 28.

Hata hivyo, Kiba katika ujumbe wake huo hakumhusisha Diamond moja kwa moja, badala yake alitaja jina la Sadala na kumfananisha kama mtu anayejidanganya kuwa ni wenzake, kumbe wanamla kisogo.

"Sadala nisikilize, kati ya hao watu ambao wewe unajidanganya kuwa ni wenzako na kudanganya watu wenye ufupi wa akili, hakuna hata mmoja ametangaza ana hela akaandikwa Facebook," sehemu ya ujumbe huo umesema.


Kisha akamalizi kwa kusema "Haina haja yakulalamika sisi ukituambia kama una hela tunaamini inatosha, ila wale wana akili ndefu."

Hakuna anayejua kama Sadala ni Diamond au mtu mwingine, ila Kiba ndiye anajua ni nani aliyemlenga kumpatia ujumbe huo.

Wiki iliyopita Forbes ilitoa orodha ya wasanii 30 wenye fedha katika bara la Afrika, namba tano za juu zilishikiliwa na wanamuziki wa Afrika Magharibi.

**BASI SAWA**

## Nuh atoa ushuhuda laki moja ilivyomliza



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Nuh Mziwanda, amekumbuka balaa lilomkumba wakati wa Sikukuu ya Iddi, akisema yote yanatokana na umaarufu alionao.

Kupitia EATV, Mziwanda ametolea maelezo taarifa hiyo, akisema yeye hakuiba pesa kama inavyodaiwa ila alitakiwa kuonekana katika sherehe moja kwa gharama ya shilingi laki moja.

"Ustaa ni mzigo wa mwiba ukiubeba unaumia hata kilichoniponza kwenye hilo jambo ni mimi kuweza kusaidia kwa sababu nilikuwa natoa msaada," amesema Mziwanda.

## Morogoro kumpata nani mbabe wa dansi nchini



BENDI tatu za muziki wa dansi zinatarajia kufanya onyesho la pamoja, katika mkakati wa kurejesha muziki huo kwenye chati.

Onyesho hilo linafanyika Mei 29 siku ya Jumamosi mjini Morogoro, na kushirikisha bendi za Waluguru Original, Bogos ya jijini Dar es Salaam na Sky Melody ya Dodoma.

Akizungumza na gazeti hili, mmoja wa waandaji wa onyesho hilo, ambaye ni mkurugenzi wa bendi ya Waluguru Original, Deogratius David 'Killer Man', amesema maandalizi yanaendelea vizuri.

"Ukweli muziki wa dansi umeshuka, hivyo kuna haja ya wanamuziki kuwa na mikakati ya kuurudisha kwenye chati, ndiyo maana tunaandaa onyesha la pamoja ikiwa ni moja ya mikakati hiyo," alisema KillerMan.




# Dogo Janja afurahia namba 3650

NAMBA 3650, ina siri kubwa kwa msanii wa muziki wa kizazi kipya, Dogo Janja, ambaye yupo katika maandalizi makubwa ya kutambulisha albam yake ya pili.

Dogo Janja ambaye ameimba kwa mafanikio nyimbo kama Ngarenaro, Ukivaaje Unapendeza na Banana, atazindua albam hiyo Mei 21 mwaka huu, huku akifanya jambo la kipekee la kuwashirikisha wanawake kwenye nyimbo zake.

"Nimetimiza miaka kumi kwenye muziki, nikiwa nimedumu siku 3650 nikiwa nimetoa albam moja, nyimbo nilizorekodi 421, jumla ya shoo nilizofanya 1562," ameandika Dogo Janja.



# AngelMary ajibebisha kwa Awilo Longomba

MWIGIZAJI Angel Mary Kato, amesema ni jambo la kujivunia kufanya kazi na msanii mkubwa kama Awilo Lungomba.

Akizungumza kupitia Planet Bongo, amesema hakutegemea siku moja atacheza filamu pamoja na msanii mkubwa kama huyo, lakini sasa anaamini kila kitu kinapangwa na Mungu.

AngelMary atashiriki katika filamu iitwayo 'Life to regret' ambapo ataigiza kama Mke wa Awilo Longomba.

# Marapa dansi waliosahaulika

**Na Adam Fungamwango**

MWANZONI mwa miaka ya 2000 na kuendelea wakati muziki wa dansi ukiwa kwenye chati, mbali na waimbaji, kuliibua marapa wengi ambao walikuwa wakiweka vionjo kwenye muziki.

Baadhi ya marapa maarufu waliokuwapo ni kama hayati, Ramadhani Masanja maarufu kama Banza Stone, Msafiri Diof, Kalala Junior, Papy Kocha Mtoto wa Mfalme na wengine wengi ambao walisababisha muziki wa dansi kupendwa na mashabiki wengi.

Baadhi yao pia ni waimbaji.

Hata hivyo walikuwepo baadhi ya marapa ambao hawakuwa na majina makubwa, lakini walishiriki kutoa mchango mkubwa kwenye tasnia ya muziki wa dansi.

Marapa ambao waliokuwa hawana majina makubwa kwa sasa wamesahaulika. Hawajulikani walipo kwa mashabiki wa muziki, ingawa inawezekana wanapiga muziki hotelini, wamenzisha bendi zao au wanafanya biashara zingine huku muda wa ziada wakijishughulisha na muziki.

Leo tutawaangalia marapa ambao kwa sasa hawazungumziwi sana, na ni kwa sababu tu hawakuwa na majina makubwa sana kama wenzao, lakini walilitendea haki dansi.

**GYASON SEMSEKWA**

Ni rapa wa zamani wa bendi za Extra Bongo, African Stars 'Twanga Pepeta', na Chipolipolo. Mara ya mwisho alikuwa ameanzisha bendi yake aliyoiita Tamba Stars.

Kabla ya hapo katikati ya miaka ya 2000, alipatwa na matatizo ya uvimbe kwenye koo, lakini alipatiwa matibabu ingawa alikaa kwa muda hadi kurejea tena kwenye masuala ya muziki.

Semsekwa anakumbuwa sana kwa rapu zake zilizokuwa zikiwachizisha mashabiki ukumbini na hata redioni. Rapu hizo ni "Kichaa kapewa rungu usijaribu kupita mbele yake". Nyingine ni 'Usimuige kasuku kuongea." Ni moja kati ya rapu zilizokuwa maarufu sana za rapa huyo ambaye ni kama amesahaulika hivi.

**MUSSA KARENGA**

Huyu naye ni mmoja wa marapa mahiri ambao hawakujaliwa kupata majina makubwa.

Alikuwa akihudumu kwenye bendi ya 'TOT Plus'. Hakupata ustaa sana kutokana na marapa aliowakuta, lakini kuna kazi kubwa alizifanya kwenye baadhi ya nyimbo ikiwamo, 'Kaona mambo huyawezi."

Alirapu kipande ambacho kilipendwa sana "La Mujer de mi vida eee, erotototototo mwanamke wa maisha yangu alee erotooooo."

**KHALID CHOKORAA**

Chokoraa ni mmoja wa marapa ambao angalau yeye alipata umaarufu kudogo na hasa alipounda bendi ya 'Mapacha Watatu' na wenzake Kalala Jounior na Jose Mara.

Naye amezunguka bendi kadhaa, akitoa mchango wake. Hivi karibuni alijiingiza kwenye masumbwi, ingawa alikuwa bado hajaacha muziki. Kwa sasa hasikiki sana kama zamani.

**KALIDJO KITOKOLOLO**

Huyu ni rapa wa FM Academia (pichani). Kama humjui, basi ile rapa kali katikati ya miaka ya 2000 iliyokuwa ikiimbwa "Hii ni ajabu ya bata kutingisha bodi manyoya, mgongo tingisha mama, mgongo tingisha..." Huyu ndiye Kadjo Kitokololo. Alitikisa kwa rapa hiyo na nyingine nyingi.

Kwa sasa hasikiki tena, ingawa inawezekana bado yupo kwenye tasnia ya muziki.

**SAULO JOHN 'FERGUSON.'**

Ni mmoja wa marapa wa Twanga Pepeta na Mashujaa ambao hawakuwa na majina makubwa sana, lakini walifanya kazi kubwa sana, katikati ya marapa maarufu kama kina Msafiri Diof.

Kwa naye hasikiki sana kwenye ulimwengu wa muziki, ingawa hakuna taarifa kama anaendelea, au yuko wapi kwa sasa.





# Goma la Wachawi; Mchana usingizi, usiku kumekucha

**Na Adam Fungamwango**

UCHAWI ni dhana ya kufikirika iliyopo duniani. Ni jambo ambalo halionekana kwa kawaida. Wachawi pia ni watu ambao hawaonekani kwa macho ya kawaida hasa kwa watu wanaoamini mambo haya.

Kwa sababu ni dhana na kuna baadhi ya watu wanaamini mambo haya, kumekuwa na matukio, na habari nyingi zikihusishwa na uchawi.

Hata kwenye baadhi ya filamu, huigiza mambo hayo. Leo tunaiangalia filamu ya 'Goma la Wachawi'. Ni moja kati ya filamu zinazozungumzia visa, maisha na mikasa ya watu wanaoitwa wachawi, pamoja na madhila yanayowakuta watu ambao hawahusiki na jambo hilo.

Kashinde ni msichana mchawi ambaye aliachiwa mikoba na mama yake ambaye ameshastaafu.

Msichana huyo anaingia kwenye chama hicho na kutoa kafara watu wengi kiasi cha kufanana idadi yake na mkubwa wa kitengo hicho malkia Kalage.

Sasa ikawa ni vita ya kugombea cheo, nani awe malkia wa wachawi kati ya malkia Kalage na Kashinde.

Kila mmoja anataka ngoma ya kichawi ikapigwe nyumbani kwake. Baada ya kutokea mapigano, Kashinde anaiba ngoma ya kichawi na kumpelekea mama yake ili afiche. Pamoja na mama Kashinde kukataa kwa sababu yeye ameshastaafu, lakini baadaye alikubali kuihifadhi ngoma hiyo kwa sababu ni binti yake.

Kazi ilikuwa ni kwa malkia Kalage kuitafuta ngoma. Yeye na wachawi wenzake waligundua kuwa iko kwa mama Kashinde.

Kumbe naye mama Kashinde baada ya kupewa ngoma ile aliipeleka kwa kijana wake wa kiume Kondo.

Akamwambia akaifiche ngoma hiyo mbali na asiipige mchana kwa sababu ilipigwa mchana ni silaha, usiku ni furaha. Malkia Kalage na kundi lake wanamuua mama Kashinde baada ya kushindwa kuwapa ngoma.

Kondo naye baada ya kusikia kuwa ngoma ile ndiyo iliyosababisha mama yake kufariki akaenda nayo mbali ili kuitupa.

Anatokewa na dada yake Kashinde na kumwambia ukweli kuwa yeye ni mchawi, anatokea pia malkia Kalage na kundi lake kwa nia ya kutaka kumpora ngoma.

Kashinda anaichukua ngoma na kuipiga, ikiwa ni mchana. Wachawi wote wanakufa akiwepo yeye mwenye aliyeipiga. Anayebaki hai ni Kondo tu.

# TI sijui kama atanasuka



RAPA mkali kutoka Marekani, TI na mkewe Tiny Harris, wamewekwa katika uchunguzi mkali kutokana na madai ya unyanyasaji wa kingono na matumizi ya dawa za kulevya.

Kulingana na mtandao wa PageSix, polisi wa Los Angeles Police, wamefungua faili la uchunguzi dhidi ya mastaa hao baada ya watu wawili ambao ni wasanii wa hip-hop kulalamika waliwekewa dawa katika kinywaji na kasha kushiriki vitendo vya ngono bila hiari yao.

Inadaiwa Jane Doe akia na mpenzi wake baada ya kunywa kinywaji cha Tiny katika hoteli moja wakiwa na TI, ghafla walijisikia vibaya na kisha kushiriki ngono.



## Burna Boy, ulipofika tema mate chini

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Burna Boy, ameibua sintofahau nchini mwake kutokana na kauli yake ya kukana asili yake.

Msanii huyo kupitia mtandao wa Twitter, amesema yeye sio msanii wa Nigeria, kwani hajawahi hata kutengeneza pesa kutoka nchini humo.

Watu waliigombania akaunti yake baada ya kauli hiyo, wengi walimuita msaliti baada ya kuendelea kushikilia msimamo wake huo.

Hata hivyo, Burna Boy, alizidi kusisitiza kuwa haipaswi kuhudumiwa kama raia wa Nigeria kutokana tu ana familia na mashabiki, vinginevyo haipendi nchi hiyo.

## Trevor amwacha mpenzi wake

MSANII wa ucheshi kutoka Afrika Kusini, Trevor Noah na mpenzi wake wa siku nyingi, Minka Kelly, wamebwagana rasmi.

Kwa mujibu wa watu wake wa karibu, wawili hao ambao wanaandaa kipindi cha 'Daily Show' wamevunja uhusiano wao kwa muda wa mwezi mmoja sasa.

Kwa mara ya kwanza wapenzi hao walikutana na kuanzisha uhusiano wa kimapenzi mwaka 2020, hata hivyo wote hawajajitokeza hadharani kuzungumzia suala hilo.





## Ariana afunga ndoa kiaina

MWANAMUZIKI wa Marekani, Ariana Grandem, amefunga ndoa na mpenzi wake Dalton Gomez, katika harusi iliyofanyika kwa usiri mkubwa.

Kulingana na watu wake wakaribu, wawili hao walifunga ndoa hiyo ambayo ilihudhuriwa na watu wasiopungua 20 pelee.

"Ilikuwa sherehe ndogo ya watu 20. Chumbani kuliwa na hali ya furaha na mapenzi tele, maharusi na familia zao walijaa furaha," kilisema chanzo.

## Naomi Campbell apata miujiza

HAKIKA Mungu akitaka kukupa hachagui siku, kwani hata ukiwa mzee au unachungulia kaburi kile alichopanga kupata ni lazima ukipate.

Wiki hii dunia ilipatwa na mshangao baada ya mwanamitindo mkongwe wa Uingereza. Naomi Campbell, kutangaza amepata mtoto akiwa na umri wa miaka 50.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Naomi alitangaza habari hiyo njema kwamba baada ya kukaa miaka yote hiyo bila kuitwa mama, hatimaye amebarikiwa kujifungua mtoto wake wa kwanza.

Mwanamitindo huyo kwa miaka kadhaa amekuwa akipigania kupata mtoto, lakini alikata tamaa kutokana na umri wake kuzidi kumtupa mkono.



MAKALA

## MAPIGANO GAZA

# Kwa nini Marekani inaitetea Israel?

Na Mwandishi Wetu

WANANCHI wa Gaza pengine wameanza kupata ahueni baada ya mapigano makali kati ya wapiganaji wa Hamas na wanajeshi wa Israel, kusitishwa rasmi jana.

Israel imeukubali mpango wa Misri wa kusitisha mapigano mabaya zaidi kuwahi kutokea tangu mwaka 2014, na imekubali bila masharti yoyote.

Misri sasa inatarajiwa kutuma wajumbe nchini Israel na Ukanda wa Gaza katika siku chache zijazo kwa lengo la kuumaliza kabisa mgogoro huo.

Hata hivyo, Hamas wanasema huenda makubaliano ya sasa yakawa na nguvu ikiwa tu Israel itaacha kutumia nguvu katika masuala ambayo yanahitaji diplomasia.

Israel nayo imeitaka Hamas kushauriana vyema na mamlaka ya Palestina ili kunusuru machafuko mengine.

Katika mpango huo wa usitishaji mapigano, nchi kadhaa zimehusika katika majadiliano hayo ya muda mrefu ikiwamo Marekani.

Rais wa Marekani, Joe Biden, amepongeza hatua ya kusitishaji mapigano hayo na kutaka pande mbili kuepuka mambo yatakayowaingiza katika vurugu.

Hata hivyo, akaitetea Israel kuwa ina haki ya kujilinda na maroketi yanayorushwa na Hamas, lakini alisita kuzungumzia uharibifu uliofanywa ukanda wa Gaza.

Je, ni kwa nini Marekani inakuwa kimya inapotokea mapigano kati ya Israel na Palestina? Haya ni baadhi ya mambo yanayosababisha serikali ya Marekani, kuwa na kigugumizi.



Makazi ya Wapalestina mjini Gaza yakishambuliwa kwa mabomu na ndege za Israel. **PICHA: AFP**

### URAFIKI WA VIONGOZI

Uhusiano kati ya Marekani na Israel ulianza muda mrefu kuanzia enzi za Rais Harry Truman, ambaye alikuwa kiongozi wa kwanza duniani kuitambua Israel kama nchi huru mwaka wa 1948.

Truman, alikuwa na uhusiano wa karibu na pia mshirika wa kibiashara wa Edward Jacobson, ambaye alichangia kuisaidia Israel itambuliwe na Marekani.

Tangu Israel ijipe uthibiti wa kijeshi kupitia ushindi wake wa vita vya 1967, dhidi ya nchi za kiarabu kama vile Misri, Syria na Jordan, Marekani iliboresha uhusiano wake na nchi hiyo na kuanza kuipa misaada ya kila aina.

### MISAADA YA KIJESHI

Israel imekuwa ikipewa misaada ya kifedha na Marekani kwa muda mrefu na hilo limekuwa likifanyika tangu vita vya pili vya dunia.

Mfano mwaka wa 2016, Rais wa Marekani wakati huo Barack Obama, alisaini mkataba wa ulinzi wa Dola bilioni 386 kuisaidia Israel, pamoja na ufadhili wa miaka 10 wa mfumo wao wa kujilinda dhidi ya makombora wa 'Irone Dome'.

Licha ya nchi hiyo kuwa na uwezo wa kiuchumi, wengi hushangaa kwa nini Marekani inawapa misaada mikubwa kama huo wa ulinzi.

Tayari teknolojia ya Israel imeimarika sana katika sekta zote, lakini inazidi kupata usaidizi wa kila aina kutoka kwa Marekani.

### MAONI YA WAMAREKANI

Maoni ya raia wengi nchini Marekani yamekuwa ya kupendelea Waisrael kutokana na kupata huduma za kampuni zenye uhusiano wa Israel na umma.



Wanajeshi wa Israel wakimdhibiti kijana wa Kipalestina katika vurugu zilizoibuka hivi karibuni. **PICHA: BBC**

Israel pia inapata huruma kutoka kwa Wamarekani ambao wameshuhudia matukio kadhaa ya kigaidi, kama shambulizi la Munich nchini Ujerumani, mwaka wa 1972, ambapo wanamichezo 11 wa Israel waliuawa na kikundi cha Kipalestina na mwaka 1976 pale Waisraeli walipotekwa katika Uwanja wa Ndege wa Entebbe nchini Uganda.

Hata hivyo, kulingana na kura mbalimbali za maoni kutoka kwa kampuni ya Gallup, Wamareani pia wameanza kuwahurumia Wapalestina baada ya kufahamu mateso wanayopitia chini ya utawala wa Israel.

### MASHIRIKA YENYE USHAWISHI

Kuna mashirika mengi nchini Marekani ambayo hutetea maslahi ya Israel, mfano American Israel Public Affairs Committee (AIPAC).

Wanachama wa kundi hilo wanaripotiwa kuwa na ushawishi kisiasa na hupata kila aina ya misaada kwa Wayahudi wa kimarekani na makanisa ya kiebanjelisti.

Rais wa sasa Joe Biden, na mtangulizi wake Donald Trump, wamewahi kwenda katika mikutano na waziri mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, iliyoandaliwa na shirika hilo.

### UKARIBU WA KISIASA

Makundi yanayounga mkono maslahi ya Israel, yanatoa mamilioni ya dola kwa wagombea wa kisiasa nchini Marekani.

Katika kampeni ya mwaka 2020, vikundi vinavyounga mkono Israel, vilitoa jumla ya dola milioni 30.95, sawa na asilimia 63 kwa Chama cha Democrats na asilimia 36 kwa Republican.

Wanasiasa wengi katika bunge la Marekani kutoka vyama vya democrat na Republican wanaiunga mkono Israel.



Makazi ya Wapalestina mjini Gaza yakishambuliwa

# Mgogoro ardhi unavyotishia amani wananchi wa Kibaha

**Na Faustine Feliciane,** KIBAHA



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, akitoa maelekezo wakati akitatua moja ya migogoro ya ardhi Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MIGOGORO ya ardhi hapa nchini imekuwa chanzo cha kusuasua kwa maendeleo katika baadhi ya maeneo kutokana na vuta nikuvute baina ya pande mbili zinazogombania ardhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Katika kipindi cha hivi karibuni kumeibuka na migogoro mingi ya ardhi, licha ya juhudi za serikali kupitia kwa wizara husika kupambana kuondoa kero hizo.

Hivi karibuni kumeibuka mgogoro mkubwa wa kugombea ardhi katika Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, kwenye vijiji vya Madabala na Mbawawa ambao imesababisha suala hilo kufika mahakamani.

Wakazi na wakulima wa vijiji hivyo, wamelalamika kitendo cha serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha, kugawa maeneo ya wakazi hao ambao wamedai wamekuwa wakiyatumia zaidi ya miaka 30 sasa.

Mmoja wa wawakilishi wa wananchi, Ally Abdallah Kawanda, aliwaambia waandishi wa habari waliokwenda katika maeneo hayo kuwa wananyanyaswa katika maaneo ambayo wamekuwa wakiyatumia kwa miaka mingi.

"Kinachotushangaza, haya maeneo yetu baadhi yamepimwa na serikali na watu wameyaendeleza kwa kilimo na wengine kujenga, lakini ghafla tunaambiwa kuna mwekezaji ambaye anamiliki eneo hili kwa halali kabisa, tunashangazwa zaidi na namna ambavyo Jeshi la Polisi linavyotufanyia kwa kumsaidia mwekezaji huyo," anasema Kawanda.

Anasema wanashangazwa kuona na licha ya mgogoro huo umefikishwa mahakamani, bado wanazidi kuwaondoa. Mkazi mwingine wa eneo hilo, Consolata Emmannuel, anaeleza sasa wamefikia hatua ya kukamatwa na Polisi pale wanapotaka kuendeleza kwa kulima au kujenga nyumba.

"Hivi karibuni baadhi ya wananchi na wakazi wenzetu wa hapa Madabala Mbwawa walishikiliwa na Polisi kwa siku kadhaa kabla ya kuachiwa kwa kosa linalotajwa kuwa kujenga na kukata miti kwenye eneo la mwekezaji," anasema Consolata.

Anaeleza kwamba kwa sasa matumaini yao ya kuendelea kukaa kwa amani na kuendelea na shughuli zao, yamebaki kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri hawajatusaidia lolote, tunamwomba aje aingilie kati, ili haki itendeke lakini tunaomba hata Rais wetu alione hili, wananchi wake tunapata shida," anaongeza kusema Consolata.

Wananchi hao wanasema wanashangazwa kuona ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha inaendelea kutangaza kuuza viwanja katika maeneo yao wakati ikijua kuna mgogoro unaendelea.

"Matangazo haya tunayasikia kwenye vyombo vya habari hasa radio, sasa eneo lina mgogoro inakuaje wanatangaza kuuza viwanja hivyo," alihoji Consolata.

**KIINI CHA MGOGORO**

Kwa mujibu wa wakazi hao wanadai kuwa mwaka 2010, walifunguliwa kesi wakimlalamikiwa katika baraza la ardhi na nyumba katika kata ya Visiga wakidai kukaa ndani ya yenye heka 561 kinyume na utaratibu.

Kawanda ambaye ni kiongozi wa wananchi hao, anasema mwaka 2011, walifunguliwa shtaka lingine na baada ya kupitia vielelezo, wananchi nao walishinda.

"Ilipofika Juni 15, mwaka 2015, jaji aliyekuwa akisikiliza kesi P. M. Kente alitupilia mbali kesi hiyo, nakala ya maamuzi tunayo," anasisitiza Kawanda.

Anasema ilipofika mwaka 2018 aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Asumpta Mshana akiongozana na mwekezaji (Jina limehifadhiwa) walifika kwenye makazi yao na kuamuriwa kuondoka kwa kile kilichoelezwa wamevamia eneo hilo.

"Kwa sasa shughuli zote za kimaendeleo ya wananchi zimesimama kwa sababu ya kuzuiwa kinguvu," anasema.

Anaeleza jitihada za kutaka kukutana na Waziri Lukuvi, zimeshindikana.

"Agosti 2, mwaka 2019 tulikutana sisi wananchi, serikali ya Mkoa na wilaya kutafuta suluhu, lakini hatukupata muafaka baada ya mkuu wa wilaya kueleza kuwa tumekubali kutoa ardhi yetu kwa mwekezaji," " anasema.

**OFISA ARDHI AWASHANGAA WANANCHI**

Ofisa Ardhi Kanda ya Pwani na Dar es Salaam, Lucy Kabyemero, anatolea ufafanuzi kuhusu mgogoro huo, akieleza suala hilo lilishamalizwa kwa kukabidhiwa kwa mmiliki halali wa eneo hilo.

"Ili suala lilishamalizwa, kuna mmiliki halali wa eneo hilo kwa sababu ana vielelezo vyote, tumeshazungumza na wananchi hao na kuwaeleza, tunashangaa kwa sasa wanalalamika kwenye vyombo vya habari, wanapaswa kuja ofisini kama wanataka maelezo zaidi," anasema Lucy.

Anasema ofisi zipo wazi kwa ajili ya kutoa maelezo ya kina kwa wananchi na pia kama wanaona wameonewa zipo ngazi za kufuatwa.

## Nabaki Afrika yaja na kampeni mpya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Nabaki Afrika Ltd inayosambaza na kuza bidhaa za ujenzi nchini, imezindua kampeni maalum ya uhamasishaji inayojulikana kama 'IPS NI BOMBA' yenye lengo la kutangaza mabomba ya majisafi yenye ubora.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Vatsal Shah, alisema bidhaa hiyo imekuwapo sokoni tangu mwaka 2000 na ilizinduliwa chini ya kampeni ya 'IPS IPO'.

Shah alisema kutokana na kuuzwa kwa kiwango kikubwa kwa bidhaa hiyo, kumesababisha mabomba yoyote yenye rangi ya brown katika soko la Tanzania kuitwa 'IPS'.

"Hii ni moja ya bidhaa bora katika soko letu na kampeni hii ya uhamasishaji inalenga pia kuwawezesha Watanzania kutofautisha bidhaa halisi ya IPS na ambayo siyo halisi.

"Ni muda mwafaka sasa kwa Watanzania kununua bidhaa zenye ubora kama IPS ambayo inatengenezwa Argentina na ina waranti ya miaka 50 kutokana na ubora wake," alisema.

Alibainisha kuwa IPS ni bomba pekee lenye waranti ya miaka 50, likiwa limetengenezwa kwa ubora wa kimataifa na kuipa uwezo wa kuhimili presha kubwa ya maji, chumvi na kemikali pamoja na kuhifadhi joto au baridi kwenye bomba.

Shah alisema bomba la IPS limetengenezwa katika vipimo sahihi ambavyo huwapa mafundi wakati mwepesi kwa kuwa halivujishi maji.

"Bomba la IPS lina rangi ya brown na mstari wa kijani, maandishi meupe na ili kujua bomba halisi utaona maandishi ya kispaniora - CALIDAD IPS.

Alisema bomba la IPS lina safu nne ambazo zinafanya bomba liwe bora kuliko mabomba mengine sokoni na safu hizo husaidia kulinda bomba dhidi ya miyonzi ya jua, kuweka majisafi na safu moja husaidia kuunga bomba vizuri ili maji yasivuje na pia lina plastiki ngumu ambayo haichakai.

Alisema bomba za IPS na viungio vyake zinapatikana Nabaki Afrika Ltd na katika maduka ya wasambazaji wake walioidhinishwa nchi nzima.

# Ndama awasilisha pingamizi kortini

**Na Mary Geofrey**

MSHTAKIWA Ndama Shabani, ameiomba Mahakama Kuu imwachie huru wakati ikisikiliza maombi madogo ya jinai aliyowasilisha mahakamani.

Ndama amewasilisha maombi hayo akitaka mahakama hiyo iangalie uhalali wa mashtaka katika kesi ya Uhujumu Uchumi namba 17/2021 aliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Kupitia wakili wake, Peter Madeleka, Ndama alidai mahakamani huko kuwa maombi hayo yamewasilishwa mahakamani chini ya kifungu namba 372(1) cha Sheria ya Makosa ya Jinai Sura ya 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019 na kifungu namba 44(1) (a) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu (MCA) Sura ya 11 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Madeleka alidai Ndama anaiomba mahakama hiyo iitishe mwenendo wa shauri la uhujumu uchumi namba 17/2021 lililoko Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ili Mahakama Kuu ijiridhishe kuhusu uhalali na usahihi wa hayo mashtaka ya uhujumu uchumi yaliyo katika hiyo ya chini.

Wakili Madeleka aliyasema hayo mbele ya Jaji Leila Mgonya, wakati shauri hilo lilipoitishwa mahakamani huko kwa ajili ya kuangalia kama upande wa mashtaka umejibu na kuwasilisha majibu yao mahakamani.

Hata hivyo, upande wa wajibu maombi, ukiongozwa na wakili wa Serikali, Candid Nasua, ulidai wamepokea nyaraka hizo jana, hivyo hawakuweza kupata muda wa kuzipitia kwa kuwa hawakupewa hata hati ya mashtaka kuhusiana na shauri hilo, hivyo aliomba mahakama hiyo iwapatie siku tano ili waweze kupitia maombi hayo na kuyajibu.

Jaji Mgonya aliwapa siku moja upande wa wajibu maombi na kueleza kuwa siku tano walizoomba ni nyingi.

"Niseme tu siku tano ni nyingi, mimi ninawapa siku moja ambayo ni Ijumaa (jana) muwe mmeshajibu na kuwasilisha hati kinzani mahakamani hapa.

"Pia ninaagiza jalada la kesi ya uhujumu uchumi namba 17/2021 lililopo Mahakama ya Kisutu liletwe Mahakama Kuu ili niweze kupitia rekodi zilizopo ndani," aliagiza. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Mei 24 mwaka huu itakapoendelea.

Ndama anakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo ya kujipatia dola za kimarekani 150,000 kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha kiasi hicho cha fedha.



Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo wa Benki ya NBC, Raymond Urassa, akitoa elimu kwa viongozi wa vyama zaidi ya 200 vya ushirika (AMCOS), mkoani Tabora, kuhusu umuhimu wa huduma za bima, matumizi ya fedha za kigeni pamoja na utunzaji wa kumbukumbu za hesabu na matumizi sahihi ya mapato yao, ili waweze kukopesheka kwa urahisi, wakati wa mafunzo yaliyofanyika mkoani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makosa ya ukatili kijinsia yapungua Mufindi

**Na Friday Simbaya,** MUFINDI

IMEELEZWA kuwa makosa ya kingono, ubakaji na ulawiti yamepungua kwa kiasi fulani katika Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa, kutokana na elimu inayohusu mambo ya ukatili inayotolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi katika Wilaya ya Mufindi, Inspekta Mary Haule wakati wa mafunzo kwa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto ngazi ya vijiji, kuhusu mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) ulioanza kutekelezwa Julai 2017 hadi Juni 2022.

Alisema makosa ya kingono, ubakaji na ulawiti wilayani humo yameanza kupungua kwa kiasi fulani na kwamba kasi ya kuripoti matukio ya mimba kwa wanafunzi imeongezeka kuanzia mwaka jana hadi mwaka huu, kutokana na janga la corona lililosababisha wanafunzi kukaa nyumbani muda mrefu.

Haule alielezea pia kuwa mashambulizi ya mke na mume na kutelekeza familia katika Wilaya ya Mufindi yameripotiwa kupungua kwa kiasi, kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau wanaofanya kazi wilayani humo. Halmashauri ya Wilaya Mufindi kwa kushirikiana na Shiriki la Umoja Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake (UN-WOMEN) pamoja na kampuni ya chai ya UNILEVER Tanzania wameendesha mafunzo hayo kwa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto katika kata saba za Igowole, Kasanga, Mninga, Mdabulo, Luhunga, Mtwango na Ifwagi wilayani humo.

Mafunzo ya kamati za ulinzi wa wanawake na watoto, yalifunguliwa rasmi na mwakilishi UN-WOMEN, Lucy Tesha, katika kata ya Igowole katika ngazi ya kijiji.

MTAKUWWA ni mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambao umeanza kutekelezwa kuanzia Julai mwaka 2017 hadi Juni mwaka 2022, ambapo unalenga kutekeleza azma ya serikali ya kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambao ni ukatili wa kingono, kimwili, kihisia na kiuchumi.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Mufindi, Sechelela Dagaa, aliainisha maeneo ya utekelezaji ya MTAKUWWA ni kuimarisha uchumi wa kaya, mila na desturi, mazingira salama, malezi, kuimarisha mahusiano na kuziwezehsa familia, utekelezaji na usimamizi wa sheri, utoaji wa huduma kwa waathirika wa ukatili, mazingira salama shuleni na stadi za maisha pamoja na uratibu, ufuatiliaji na tathmini.

Mafunzo hayo ya MTAKUWWA yanatolewa katika kata saba kati ya 27 za Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi pamoja na vijiji zaidi ya 33, ili kubaini uelewa wao kuhusu mada husika za kumlinda mama na mtoto, pamoja na kujadili baadhi ya changamoto zilizopo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## SHAMBA LINAUZWA MKULAZI

NGERENGERE ZIPO HEKA 200, UMBALI NI KILOMETA 150 KUTOKA MSAMVU ROUND ABOUT MOROGORO.
KWA MAWASILIANO;
0786051515-MUSTAQIM
0717875755-CHARTON

**Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SHANI JACKSON LUDIGIJA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA MARK 11 yenye namba za usajili T 383 BCM.Chassis No.GX-1000012488,Engine No.1G6422492. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi DSM /PHQ/R-B/249621/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

KAHAMA IMPORT AND EXPORT
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC.759 AJV, yenye Chassis no. LTZPC-JLN7F6200039, Engine no. 156FMIF0000674
Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake,
Taarifa ya jeshi la polisi,
KAH/RB/TR/207/2021.

## KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

**HATI NAMBA**; 9159

**MMILIKAJI:** THE REGISTERED TRUSTEES OF MOROVIAN CHURCH IN SOUTH WEST TANZANIA REGISTERED TRUSTEES of P. O BOX 138,MBEYA,

**MWOMBAJI:** EDSON MWAKABENGA LINOGILE AND ASULUMENTE HASAN MWAANGAYA of P.O BOX 370, MBEYA,

**ARDHI:** L.O.NO 144073, Kiwanja na. 24, Kitalu `EE, Iyunga, Mbeya Mjini,
**ENEO;** Meta za Mraba, 4922,

TAARIFA IMETOLEWA kwamba hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna pingamizi kwa muda wa mwezi mmoja tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la serikali.

Hati ya asili ikionekana irudishwe kwa Msajili wa Hati Msaidizi Mkuu, S.L.P. 2984, Mbeya.

**S.I.Diombanya
MSAJILI WA HATI MSAIDIZI
MBEYA-MKOA
19 May, 2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

RICHARD MAJENGA
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.542 DDN, aina ya NOAH.
Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake,
Taarifa ya jeshi la polisi,
KAH/RB/TR/202/2021.

**Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie
0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# Aolewe au afe-7

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho.

Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini.

Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

**Na Adam Fungamwangwo, (0716 350534)**




"Nyamaza wewe, sivyo nitakuua na hakuna mtu yoyote atanifunga. Kijiji kimeshawachoka. Ndiyo kwanza watafurahi wewe kufa. Watu watafanya sherehe na kunipongeza. Hakuna anayekutaka wewe hapa kijijini. Umewakwanza wengi sana."

Bishada alitetemeka. Hakujua la kufanya. Alijua akipanua domo lake tu, basi panga lile butu litaishia mwilini. Hakujua afanye nini. Kukimbia itakuwa ni kujidanganya. Alijua asingeweza kufika hata hatua ishirini kabla ya kukamatwa na hiyo ingekuwa hatari zaidi kwake.

Alichokuwa anaombea hapo kutokee mtu yoyote ambaye anakuja kisimani. Haikuwa hivyo Hakukuwa na dalili yoyote ya mtu.

Deo kijana wa kijiji hapo alimkamata mkono kwa nguvu, huku uliobaki ukiwa ameshika panga.

"Nifuate huku." Kitendo kilifuatiwa na maneno.

Bishada alipelekwa sehemu ambayo si njia ya kwenda nyumbani au kurudi. Bali walikatisha kuelekea porini. Sehemu ambayo watu hawapiti.

Deo aliporidhika na sehemu ila alisimama na kumuachia mkono.

"Sasa ili nisikudhuru au kukumaliza, vua nguo mwenyewe. Nimekutongoza sana, unajifanya bonge la mrembo, kila mtu hapa kijijini umemkataa. Hata kuolewa unakataa. Sasa leo umepatikana."

"Sitaki."

"Weee, nimekwambiaje? Nitakutia panga wewe." Akasema huku akiinua panga lake juu kumtishia.

"Basi navua." Bishada alisema huku akiteteka. Kabla hajajua nini cha kufanya alipigwa vibao viwili vya nguvu ambavyo vilimvuruga kabisa.

"Fanya haraka."

Hakuwa na jinsi. Alitekeleza maagizo ili mradi tu asimdhuru au kumuua.

"Ukifanya ninavyotaka nitakuachia, ila usimwambia mtu." Deo alisitiza.

Deo alipagawishwa na mwili mororo wa msichana huyo. Alikuwa anaona tu sura yake na urembo, lakini hakuwahi kuona mwili wake.

Udenda ulimtoka. Wakati Bishada alitoa nguo zake moja baada ya nyingine. Deo naye alianza kuchojoa suruali yake. "Mtoto mzuri kama wewe, unakataa wanaume kaka sisi."

Mate yalimtoka Deo. macho yake yalikuwa yakiendelea kupagawishwa na Bishada.

Akili ikampaa. Sasa kazi iliyokuwa imebaki ni moja tu. Kabla hajafanya chochote kile alishtukia akirushwa hapo alipo na kudondokea mbali, baada ya kupigwa na kitu kizito kwenye taya.

"Unataka kufanya nini hapo?"

Aligeuza shingo kuangalia kitu kilichomrusha kama gunia.

Macho yake yalikutana na jamaa mmoja ambaye alionekana ni mkubwa kuliko yeye.

Alionekana kuwa na miaka ipatayo 34 hivi. Alivaa jeans ya mpya ya bluu, pamoja na fulana nyeusi ya mikono mirefu.

Wajihi wake ulikuwa ni mrefu, mwembemba, lakini akionekana ni mkakamavu.

Kitu pekee ambacho Deo aliamini ni kwamba hakuna mtu wa kijijini hapo Mtakuja.

Alikuwa mgeni. Tena wala si mwenyeji wa kijijini cha jirani. Kifupi tu ni kwamba alionekana ametoka mbali.

"Mbona hunijibu? Ulitaka kumfanya nini?"

Wakati huo Bishada alikuwa ameshafumba macho. Kitu ambacho alitarajia ni ukatili na maumivu yasiyosemekana. Na hii yote ilikuwa ni kutaka tu kuponyesha roho yake.

Badala ya kile alichotarajia alisikia kitu kama kimetupwa pembeni yake. Alifumbua macho kwa mbali. Hakumuona mtu ambaye sekunde chache zilizopita alikuwa akitamba na kutaka kumfanyia ukatili.

Aliyesimama ni mtu mwingine ambaye hamfahamu. Hakuwahi kumuona kabla. Woga ulifanya aibu iondoke.

"Vaa nguo zako dada." Alisikia sauti hiyo ilimwambia, ikiwa imebadilika ghafla kutoka ile ya ukali, hadi ya kusihi.

Ndipo alipokumbuka kuwa hakuwa na nguo. Zilikuwa pembeni. Huko huko ndipo alipomuona Deo akiwa ameanguka. Alikuwa anajitahidi kuinuka na kutaka kukimbia.

Jamaa alimfuata, akamkamata na kumshindilia ngumi nyingine ya taya kwa ajili ya kumchanganya akili.

Deo alipepesuka. Alijikuta akichotwa mtama uliiompeleka chini.

Ndipo alipogundua kuwa jamaa aliyemfuma hapo alikuwa mahiri na isingekuwa rahisi sana kumkimbia.

"Bibie kakate kamba kwenye mti ule uniletee haraka."

Bishada kwa haraka akimbia kwenda kuchuma kamba. Hakutaka kupinga chochote alichoambiwa na jamaa yule mgeni kwa sababu alionekana ni mtu mwema kwake kuliko mtu ambaye anayemfahamu.

Alipozileta alimkabidhi na akuangalia nini kinafuatia. Kamba zile alifungwa Deo. Alifunga mikononi kama pingu.

"Hapa si ndiyo kijijini kwenu?" Mgeni aliuliza.

"Ndiyo." Bishada alijibu.

"Haya tunaenda na huyu hadi kwa Mwenyekiti wa Kijiji halafu utakwenda kusema jinsi gani alitaka kukufanya, sawa?"

Bishada aliitikia kwa kichwa.

******************************

Habari zile zilienea haraka kijijini hapo. Mtu mmoja mgeni ambaye hakujulikana wapi ametokea, kuzima jaribio la Bishada kubakwa na Deo.

Kesi isingekuwa kubwa sana kama asingeletwa na mtu yule. Ni kwa sababu hata Mwenyekiti alikuwa mmoja wa watu ambaye alikuwa haipendi familia ya mzee Ngoma ambaye ni baba yake Bishada.

Hata hivyo alilazimika kutokana na kwamba imeletwa na jamaa ambaye alikuwa amefikia kijijini hapo.

Mgeni yule si mwingine ila ni Denis au mwenyewe alipenda kujiita Denny. Alifika kijijini hapo kwa sababu maalum. Alikuja kuangalia mali za mjomba wake aliyefariki miaka miwili iliyopita.

Mjomba wake mzee Malilo hakuacha mke wala mtoto, hivyo alimundikisha yeye mtoto wa dada yake kuwa ndiye mrithi wa mashamba yake 10 yaliyopo kijijini hapo.

"Mama yule unamjua?"

"Ndiyo. Ni mpwa wa marehemu mzee Malilo, si unaona amefikia kwenye nyumba yake."

"Umeshawahi kumuona kabla?"

"Alishawahi kuja hapa bado mdogo tu, mimi nilikuwa na mimba yako."

"Kukosa yule mwanaume mama nadhani saa hizi ningekuwa nimeshajiua. Nisingekubali kufanyiwa vile halafu niendelee kuwa hai."

"Usiseme hivyo mwanangu, haya yote mambo yanapangwa na Mungu. Kwanza inabidi tumwite ili tumpe shukurani, maana tangu jana kule kwenye Ofisi za Kijiji tulipoachana naye hadi leo hatujamuona."

"Nitaenda kumwita."

"Nani wewe."

"Mimi ndiyo." Bishada alimjibu mama yake huku akitabasamu.

Mama yake alimuangalia usoni binti yake akatabasamu pia.

"Kamwite aje kula chakula cha mchana."

"Kwanza tumchinjie kuku. Yule kuku wangu mmoja, ngoja nimwite mzee Kibedi amchinje kwa ajili ya mgeni."

"Na Mpunga ule tuliounika juzi si upo, tuutwange tumpikie. Na hii itakuwa ni shukrani kubwa kwetu, maana hatuna cha kumpa."

"Kwani yule mgeni ametokea wapi?"

"We mwana we mbona unaniuliza hivyo? Si itakuja mwanangu utamuuliza? Au ukienda kumwita muulize mwenyewe. Wewe ndiyo itatuambia alikotokea."

Kwa mbali, Bishada alianza kuhisi kitu ambacho hakuwahi kuhisi huko nyuma. Hakujua ni nini.

***Itaendelea Jumamosi***

# MARCELO AKATALIWA INTER MIAMI




**MIAMI,** Marekani

KOCHA wa Inter Miami, Phil Neville amekanusha uvumi kwamba, miamba hao wa Ligi Kuu Marekani (MLS), wanataka kumsajili nyota wa Real Madrid, Marcelo.

Mkataba wa Marcelo unamalizika mwaka 2022, lakini beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 33 majaliwa yake hayajulikani kwa miamba hao wa LaLiga kutokana na kiwango chake kushuka.

Inter Miami, ambayo mmiliki mwenza wake ni nyota wa zamani wa Madrid, David Beckham, pamoja na kuhusishwa na Marcelo - pia wanatajwa kuwahitaji Gonzalo Higuain na Blaise Matuidi.

Nahodha wa sasa wa Madrid, Sergio Ramos, ambaye atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu, pia ameripotiwa kuwa kwenye rada za Inter Miami. Hata hivyo, Neville 'amemmwagia maji ya baridi' kuhusu uvumi huo kuhusu kuhusishwa na mkongwe huyo wa Brazil.

"Sioni kama kuna uhitaji wa mlinzi mwingine wa kushoto," amesema Neville ambaye ni mchezaji wa zamani wa Manchester United akiwaambia waandishi wa habari.

"Nina walinzi wengi wa kushoto, kwa hiyo sidhani kama tutakuwa tunamhitaji kwenye kikosi chetu kwa sasa."



# Casillas aibuka kumtetea Zidane

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane hapaswi kulaumiwa na yoyote kama Real Madrid watashindwa kushinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu, kwa mujibu wa golikipa wa zamani wa timu hiyo, Iker Casillas.

Madrid wamepitwa pointi mbili nyuma ya vinara Atletico Madrid wakati leo zikichezwa mechi za mwisho za ligi hiyo kwa msimu huu.

Atletico watacheza na Real Valladolid ambao wapo kwenye hatari ya kushuka daraja huku Madrid watakuwa nyumbani kucheza na Villarreal waliopo nafasi ya saba. Kama Atletico watashinda ubingwa wa LaLiga inamaanisha Madrid msimu huu itakuwa imemaliza bila taji kubwa, na kumekuwa na uvumi kuhusu majaliwa kocha wake mkuu, Zidane.

Hata hivyo, Casillas amedai mchezaji mwenzake huyo wa Madrid hapaswi kulaumiwa kama wakishindwa kubeba taji hilo msimu huu.

Zidane ameshinda mara mbili taji la LaLiga na mara tatu mfululizo Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na Supercopa, UEFA Super na Klabu Bingwa ya Dunia mara mbili.

"Zidane hatakiwi kushutumiwa kwa chochote," amesema Casillas, ambaye aliichezea klabu hiyo mechi 510 kwenye LaLiga, akiiambia redio Marca.

"Kile alichofanikiwa ni kikubwa, na hatakiwi kwa sasa kulaumiwa kuhusu kushindwa kubeba taji."

# 'Uhamisho wa Kane Man City utakuwa mgumu'

**MANCHESTER,** England

GWIJI wa Manchester City, Francis Lee, amesema uhamisho wa Harry Kane unaweza kuwa "mgumu sana" wakati akiuliza kama nyota huyo wa England anaweza kuwa suluhisho la kudumu.

Kane ameonyesha ishara ya dhati kwamba anataka kuondoka Tottenham mwishoni mwa msimu huu, akibainisha kwamba anataka kushinda mataji.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England, Manchester City wanaonekana kuwa na nafasi kubwa ya kumsajili Kane ambaye pia anahusishwa na Chelsea na Manchester United.

Kane, ambaye atatimiza umri wa miaka 28 ifikapo Julai, mwaka huu yupo sawa na Mohamed Salah katika idadi ya mabao waliyofunga wakati Ligi Kuu England ikiwa kwenye wiki yake ya mwisho msimu huu.

Hofu kubwa imebaki ni kiasi gani cha fedha kinaweza kumshawishi straika huyo kujiunga na City na Lee anaona kuwa usajili huyo unaweza kuwa mgumu sana.

"Kuna wachezaji watatu au wanne wanaoweza kufiti na kuwa mbadala wa muda mrefu kwa City," amesema Lee akiiambia Stats Perform.

Yeye kwa upande wake anawaona nyota wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 20, Erling Haaland na kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish kuwa ndio wanaweza kuwa suluhisho la kudumu kwa City.

"Inaweza kuwa ni ngumu sana kwa Harry Kane kuhamia Manchester City kwa sababu usajili wake utahitaji fedha nyingi sana," ameongeza Lee.



HABARI MICHEZO

# Diogo Jota aimarika kuelekea euro 2020

**LISBON,** Ureno

KOCHA wa Ureno, Fernando Santos anajiamini kwamba, Diogo Jota atakuwa fiti kuichezea timu hiyo kwenye michuano ya Euro 2020, licha ya fowadi huyo wa Liverpool kuwa majeruhi baada ya kuumia mguu.

Jota alipata majeruhi hayo wiki iliyopita wakati wakishinda mabao 4-2 dhidi ya Manchester United pale Old Trafford – mchezo ambao alifunga na amekosa mechi mbili za wekundu hao.

Hata hivyo, Klopp amebainisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ana nafasi ndogo ya kurudi kwenye mchezo wa mwisho wa kesho Jumapili dhidi ya Crystal Palace.

Baada ya kutajwa kwenye kikosi cha Ureno cha wachezaji 26 tayari kwa ajili ya michuano hiyo mwezi ujao, Santos amethibitisha Jota ataweza kuwa fiti kwa ajili ya michuano hiyo.

"Taarifa nilizonazo ni kwamba atakuwa fiti na anaweza kuanza mazoezi na wachezaji wenzake," alisema Santos akiwaambia waandishi wa habari.

"Nimewaambia maendeleo yake ni mazuri na kwa namna yoyote ninajiamini anaweza kuwa fiti kwa ajili ya michuano hii."

Jota amekuwa na mwanzo mzuri pale Liverpool tangu alipotua hapo kwa pauni milioni 45 akitokea Wolves.







# BARCELONA YAJITOSA KUMSAJILI DONNARUMMA

**MILAN,** Italia

GOLIKIPA wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma amepewa ofa ya kujiunga na Barcelona na wakala wake, Mino Raiola, kwa mujibu wa Diario AS.

Majaliwa ya Donnarumma yametawala sana vyombo vya habari kutokana na kukataa kuongeza mkataba wake na klabu hiyo.

Milan walitaka kumwongezea mkataba kipa huyo wa Italia ambaye wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Na sasa Barcelona imeamua kujitosa kuwania saini ya mchezaji huyo ambaye amekuwa kwenye kiwango bora.

Licha ya Barcelona pia anahusishwa na miamba wa Italia, Juventus, Barca, Manchester United na Chelsea.

Kama Donnarumma ataweza kujiunga na Barca basi kuna uwezekano mkubwa Marc-Andre ter Stegen ambaye golikipa namba moja wa timu hiyo ataondoka.

# *Mbappe: Sijivunii kuwa mchezaji ghali*

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema hajawahi kutamba wala kuona ufahari mkubwa wa kuwa mwanasoka mwenye thamani zaidi duniani kwa sasa.

Mbappe alijiunga na Paris Saint-Germain kutoka Monaco mwaka 2017 kwa uhamisho wa fedha nyingi zaidi, huku pia akishinda mataji kadhaa za PSG na Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa mwaka 2018.

"Haingii kichwani mwangu," Mbappe aliiambia TF1 alipoulizwa juu ya kuwa mwanasoka mwenye thamani zaidi duniani.

"Sio fedha nyingi inayoingia mfukoni mwangu, na sifikirii kuhusu hilo.

"Ninajifurahisha kila siku na ninajua kuwa nina bahati sana. Ninachotaka kufanya ni kushinda. Nina furaha na maisha yangu. Wakati mwingine ningependa kuwa na utulivu, lakini ndivyo ilivyo. Kuna mazuri na mabaya, lakini nina furaha."

Mbappe atacheza pamoja na Karim Benzema kwenye mashindano ya Ulaya msimu huu wa joto, na labda katika siku za usoni huko Hispania, kama atatua pale Santiago Barnabeu.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BERGKAMP ATAKA ARSENAL IUZWE

Ameungana na Henry pamoja na Vieira katika kumshinikiza mmiliki wa klabu hiyo aiweke sokoni...

**LONDON,** England

DENNIS Bergkamp amemwonya mmiliki wa Arsenal, Stan Kroenke kwamba, Mtendaji Mkuu wa Spotify, Daniel Ek na kundi la wachezaji magwiji wa zamani wa klabu hiyo "tupo hapa kutaka" wakati wakipiganigia kuuzwa kwa klabu hiyo.

Bilionea wa Sweden, Ek alibainisha kuwa na mpango wa kutaka kuinunua Arsenal, ambayo ameishabikia tangu akiwa na umri wa miaka nane, wakati wa wiki ya kuanzishwa na kuanguka kwa Ligi mpya ya Ulaya.

Tajiri huyo mwenye umri wa miaka 38 anaungwa mkono kwa nguvu zote na wachezaji ambao ni alama ya washikabunduki hao, Bergkamp, Thierry Henry na Patrick Vieira.

**Lakini mapema wiki iliyopita, Ek alidai kwamba ofa yake ya awali ya kutaka kuinunua klabu hiyo ilikataliwa.**

Hata hivyo, Ek hajakata tamaa ya kuinunua klabu hiyo kutoka kwa Kroenke na Bergkamp - pamoja na Henry wamekuwa wakiongeza mafuta kwenye moto huo.

"Hatuwezi kumlazimisha yoyote kuuza. Naelewa hivyo," alisema Bergkamp akiiambia Voetbal International.

"Kwa nyongeza Daniel amewasiliana mara mbili na Josh Kroenke na benki.

"Vyovyote itakavyokuwa kwa Kroenke, lakini hilo halitaweza kuzuia kuinunua Arsenal.

"Sisi tupo hapa kukaa, hivyo kwa namna yoyote, lazima klabu iuzwe ili iweze kuwa kwenye nafasi nzuri ya ushindani."

## ZISIKUPITE

### KANE AGEUKA LULU

KLABU ya Manchester City wako tayari kuwashinda Manchester United na Chelsea kuipata sahihi ya mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 ambaye anasisitiza Tottenham haiwezi kumzuia kuondoka. ***(Star)***

### SPURS WAMSHANGAA KANE

WACHEZAJI wa Tottenham Hotspur, wanasemekana kushtushwa na uamuzi wa Harry Kane kujitokeza hadharani kuonyesha nia yake ya kuondoka klabuni hapo. ***(Mirror)***

### BUENDIA KUTUA ARSENAL

ARSENAL wameongeza juhudi zao kutaka kumsajili kiungo wa Argentina mwenye umri wa miaka 24, Emiliano Buendia kutoka Norwich City. ***(Mail)***

### CITY YAMBANA STERLING

MABINGWA wa Ligi Kuu England, Manchester City wamepania kumpa mshambuliaji wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26, mkataba mpya wa kudumu. ***(Telegraph)***

### BALE KUBAKIA SPURS

NYOTA wa Real Madrid na Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31, anaweza kuongeza muda wake wa mkopo na Tottenham Hotspur kwa mwaka mwingine ikiwa Harry Kane atapewa ruhusa ya kuondoka klabuni hapo. ***(AS)***

### ARMSTRONG AGOMBEWA

WEST Ham na Fulham wanaongoza harakati za kutaka kumsajili mshambuliaji wa Blackburn Rovers, Adam Armstrong, ambaye thamani yake ni pauni milioni 25, lakini klabu hizo vinakabiliwa na ushindani kutoka kwa Brighton na Everton. ***(Sun)***

### WILDER ANUKIA BROM

KLABU ya West Bromwich Albion iko tayari kuanza mazungumzo na bosi wa zamani wa Sheffield United, Chris Wilder, 53, juu ya kuchukua nafasi ya Sam Allardyce. ***(Telegraph, subscription required)***

### TUCHEL AMTAKA SULE

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel bado "ana hamu sana" kumsajili beki wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Niklas Sule, 25. ***(Abendzeitung)***

### TRAORE AFIKIRIA MKATABA

WINGA wa Wolves, Adama Traore, 25, yuko kwenye mazungumzo juu ya mkataba mpya katika klabu hiyo, huku kukiwa na uvumi wa yeye kutakiwa na Liverpool na Barcelona. ***(Goal)***

### SERGIO, BARCA SAFI

UHAMISHO wa mshambuliaji wa Argentina, Serio Aguero kwenda Barcelona kutoka Manchester City umekamilika kwa asilimia 80, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 akipangwa kufanyiwa vipimo na klabu hiyo ya Katalunya mara tu baada ya City kushiriki fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mundo Deportivo)***

## HABARI MICHEZO

# SERIKALI YAVIKUMBUSHA VYAMA KUACHA 'USANII'

**Na Saada Akida**

KATIBU Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na michezo, Dk. Hassan Abbas, amewataka viongozi wa vyama na mashirikisho mbalimbali ya michezo kuacha maneno na badala yake kuweka 'mezani' mikakati na hoja za msingi kwa ajili ya kuboresha michezo hapa nchini.

Dk. Abbas alisema hayo baada ya kufunga kozi ya uratibu wa michezo na usimamizi wa fedha michezoni, iliyosimamiwa na taasisi inayotoa elimu ya michezo ya Malya.

Kiongozi huyo alisema viongozi wa michezo wanatakiwa kutumia elimu wanayopata kwa weledi ili kukuza michezo na kuacha tabia ya kuzungumza bila ya kufanya vitendo katika vyama vyao.

Alisema viongozi wasilalamike kukosekana miundombinu ya michezo na badala yake wanatakiwa kujipanga katika kuandaa mipango ya ujenzi wa viwanja.

"Serikali yetu kwa sasa ni sikivu sana, hivyo mashirikisho na vyama vya michezo vinatakiwa kuunda hoja, kuweka mikakati madhubuti ili kukuza michezo, nina imani tutakapojenga hoja tunaweza kujenga viwanja kwa kila mchezo, lakini tukaweza kumiliki hata ndege zetu.

"Viongozi mkaitumie na kusimamia elimu mliopata ya misingi na utawala bora kwa kuheshimu katiba za vyama na mashirikisho yenu, hatutakuwa na subira wala uvumilivu kwa viongozi watakaokiuka katiba," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza bado iko haja katika kuboresha uendeshaji wa vyama ambapo kwa sasa hauridhishi na unapelekea kukosekana kwa vipaji vipya na kutokuwapo kwa wawekezaji.

Alisema pia serikali inakuja na mageuzi mengi na kuwaomba wadau kupokea mabadiliko yatakayofanywa kwa kuhakikisha mabadiliko ya michezo nchini yanaonekana kwa timu na wanamichezo kufanya vizuri na kutambulika zaidi kimataifa.



Mchezaji wa tenisi, Ali Suleiman akifanya mazoezi kwenye viwanja vya Gymkhana kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Davis yanayotarajiwa kufanyika kuanzia mapema mwezi ujao hapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NIC yajitosa Dar City Marathon

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC), limetangaza kudhamini mbio za Dar es Salaam ( Dar City Marathon), zinazotarajiwa kufanyika kesho kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja hapa jijini, imefahamika.

Mkurugenzi wa Masoko na Huduma kwa Wateja wa NIC, Isaya Mwakifulefule, alisema lengo la kudhamini mbio hizo ni kusaidia kukuza michezo na kujenga afya kwa jamii ambayo wanafanya nayo kazi.

Mwakifulefule alisema wamejiandaa kushiriki katika maendeleo ya michezo na vile vile katika shirika hilo lengo la kukuza ajira kwa vijana.

Alisema pia wanahitaji kuboresha uhusiano na wadau wao na anaamini kwa kupitia Dar City Marathon, wanariadha watakaoshiriki watajiweka imara kuelekea mashindano mengine mbalimbali ya ndani na nje ya nchi watakayokwenda kuchuana.

"NIC imeamua kushiriki kikamilifu katika mbio hizo kwa kutambua kuwa haiwezi kuiacha jamii ambayo ndio sehemu kubwa ya wadau wake na watumiaji wa bima mbalimbali," Mwakifulefule alisema.

Mratibu wa mbio hizo, Godfrey Mindu, aliwashukuru NIC kwa udhamini walioutoa ambao umekuwa na mchango mkubwa katika kuleta furaha kwa wanariadha watakaoshiriki.

"Washiriki watakaokimbia umbali wa kilomita 21 watapatiwa fulana na mshindi wa kwanza kwa wanaume atapewa zawadi ya Sh. milioni moja, mshindi wa pili Sh. 750,000, wa tatu Sh. 500,000, wanne Sh. 300,000 na watano ataondoka na Sh. 200,000, lakini wale watakaoshika nafasi ya sita hadi wa 10 kila mmoja atapatiwa Sh. 100,000," alisema Mindu.

Alitaja zawadi nyingine kwa washindi wa mbio za kilomita 10 kwa wanawake na wanaume ni Sh. 500,000 kwa mshindi wa kwanza, mshindi wa pili Sh. 375,000, mshindi watatu Sh. 250,000, wanne Sh.150,000 na watano Sh. 100,000 huku watakaoshika nafasi ya sita hadi ya 10 kila mmoja atapewa Sh. 50,000.

## Katwila arejesha matumaini Ihefu

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Ihefu SC, Zuberi Katwila, amesema bado hawajakata tamaa na malengo yao ni kuendelea kupambana na kusalia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara katika misimu mingine ijayo.

Katwila alisema hayo baada ya juzi timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji FC na kurejesha matumaini ya kujinusuru na janga ya kushuka daraja.

Kocha huyo alisema amewaandaa wachezaji wake kuendelea kupambana na hatimaye kufanya vizuri katika mechi zote nne zilizobakia ambazo watacheza ugenini.

"Lengo ni kuhakikisha timu yangu inaendelea kushiriki Ligi Kuu, nitahakikisha ninapata pointi tatu katika michezo yetu yote iliyobakia ili kumaliza msimu, tunaomba mashabiki pamoja na wadau wa Ihefu wazidi kutuunga mkono," alisema Katwila.

Hata hivyo alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri wakati walipokutana na Dodoma Jiji ambayo nayo ilihitaji ushindi.

"Mechi ilikuwa ngumu na yenye ushindani, lakini vijana walipambana na walijitahidi kulinda bao tulilopata katika kipindi cha kwanza, tutaendelea na mapambano hayo hayo," alisema kocha huyo.

## Bingwa wa misuli kupatikana Agosti

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya kusaka bingwa wa Taifa wa kujenga misuli yamepangwa kufanyika Agosti 8, mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Watunisha Misuli Tanzania (TBBF), Francis Mapugilo alisema maandalizi kuelekea mashindano hayo yako katika hatua nzuri na washiriki wanaendelea kujinoa.

Mapugilo alisema wanatarajia mashindano ya mwaka huu yatakuwa na ushindani kwa sababu ya maandalizi ya muda mrefu ambayo yamefanywa na watunisha misuli hao.

"Kwa sasa tunajiandaa na mashindano hayo ambayo yatafanyika hapa jijini Dar es Salaam, ni mashindano ambayo yatakuwa na ushindani kwa sababu kila mshiriki amejipanga kikamilifu,"alisema Mapugilo.

Kiongozi huyo alitoa shukrani kwa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), kwa ushirikiano ambao wanawapatia tangu shirikisho hilo liliponzishwa kwa kuwapa ushauri ambao unawaletea manufaa na wa kuendeleza mchezo huo.

# Michezo

Jumamosi Mei 22, 2021

Nipashe




Marcelo akataliwa Inter Miami

UKURASA 20



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (kulia), akipambana kuwania mpira katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa kuwakaribisha Kaizer Chiefs katika mechi ya marudiano ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo jijini Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yamweka kitimoto Lamine

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu yao ikihitaji kikosi imara kuelekea hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mabosi wa Yanga wanatarajia kutoa msimamo wao kuhusiana na kurejea kambini beki Lamine Moro ambaye alisimamishwa kutokana na utovu wa nidhamu.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema uongozi wa klabu hiyo ilikuwa na kikao na benchi la ufundi ambalo ndilo lililomwondoa beki huyo raia wa Ghana halafu pia itakutana na nyota huyo ili kufikia mwafaka.

"Ni kweli kulikuwa na kikao na benchi la ufundi, lakini mchezaji mwenyewe. Uongozi umekutana na pande zote mbili kama ilivyo kawaida kama unataka kusuluhisha kwa haki, lazima ukutane na pande zote. Majadiliano yamefanyika na yamepelekwa tena kwenye benchi la ufundi, lakini klabu itatoa msimamo hivi karibuni, wanachama na mashabiki wa Yanga wasiwe na wasiwasi," alisema Bumbuli.

Kiongozi huyo alisema mchezaji huyo hadai chochote kama baadhi ya taarifa zilivyoandika (sio Nipashe), na sababu ya kutoonekana kambini ni kusimamishwa na benchi la ufundi.

Bumbuli pia alitangaza rasmi kuwa mchezaji wao mareruhi wa muda mrefu, Mapinduzi Balama amepona na ataungana na wenzake hivi karibuni huku Yassin Mustapha, Abdallah Shaibu 'Ninja' na Carlos Carlinhos ambao walikuwa majeruhi afya zao zimeimarika na watarejea kwenye mapambano.

# Simba yajipanga kufanya maajabu

**Na Saada Akida**

## ●●● Kocha Gomes asema hakuna kinachoshindikana, ulinzi mkali kambi ya wapinzani wao...

USIKU wa deni haukawii. Ni ile siku ambayo wanachama na mashabiki wa Simba walikuwa wanaisubiri wakati timu yao itakapoikaribisha Kaizer Chiefs katika mechi ya marudiano ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Simba itashuka uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa mabao 4-0 katika mchezo wa kwanza uliochezwa wiki iliyopita jijini Johannesburg, nchini Afrika Kusini.**

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes alisema Kaizer Chiefs sio timu bora sana ila 'walimwahi' katika mchezo wa kwanza na sasa wako tayari kuwaonyesha uwezo wao katika mechi ya leo.

Gomes alisema Kaizer Chiefs hawakuwa bora ukilinganisha na timu nyingine walizokutana nazo katika michuano hiyo, ila wapinzani walitumia vyema nafasi waliyopata na kuondoka na ushindi mnono, lakini kikosi chake kina matarajio makubwa ya kusawazisha makosa yake.

Mfaransa huyo alisema timu zote ni nzuri kwa sababu wamefika hatua ya robo fainali na 'anawaita' leo uwanjani kwa ajili ya kupambana na hatimaye 'kupindua' matokeo ya mechi iliyopita.

"Tumejiandaa vizuri na kikosi kipo imara, tutamkosa kiungo wetu, Jonas Mkude ambaye amekuwa na shida kidogo ila waliobakia wote wako fiti kwa ajili ya 'kupindua matokeo'. Tuna waheshimu Kaizer Chiefs na tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu ili kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kupata ushindi na kusonga mbele katika michuano hiyo," alisema Gomes.

Alisema watashuka dimbani kwa ajili ya kupambana na kuhakikisha hawawaangushi mashabiki wao ambao wamekuwa na imani na timu hiyo tangu ilipoanza kupeperusha bendera katika michuano hiyo ya Afrika.

Aliongeza wachezaji wana morali nzuri na kila mmoja na ari ya kutaka kupata ushindi huku wakiamini uwezo wa kushinda mabao 5-0 katika uwanja wao wa nyumbani wanao.

"Tulipata nafasi ya kuangalia mapungufu yetu, nami binafsi niliutazama mchezo ule mara mbili, hivyo tayari tumefanyia marekebisho matatizo yetu. Naamini kama hatutarudia makosa na tukajitoa kwa uwezo wetu wote bila shaka hakuna kinachoshindikana, tunajiamini kuwa tunayo nafasi kubwa ya kuweza kupindua matokeo.

"Sijui nini kitatokea Jumamosi (leo), lakini najua tutashinda na tutatumia mbinu tofauti kabisa kumaliza mchezo. Kesho tutacheza kufa na kupona, wachezaji wapo tayari kupambana, wapo tayari kufanya maajabu, hakuna kinachoshindikana," Gomes aliongeza.

Nahodha na mshambuliaji wa Simba, John Bocco, aliliambia gazeti hili kikosi cha timu hiyo kinaamini kitapata matokeo mazuri na hawajakata tamaa.

"Kwanza tunamshukuru Mungu tumefanya mazoezi vizuri tangu tuliporejea, hatuna tatizo lolote, kwa kifupi niseme hatujakata tamaa, tunajiamini tunakwenda kupata ushindi," Bocco alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ambaye ndiye mgeni rasmi katika mechi ya leo amewataka mashabiki wa soka jijini kuacha tofauti zao na kujitokeza kwa wingi kuwashangilia Simba ambayo inawakilisha nchi katika michuano hiyo.

Makalla alisema kufanya vizuri kwa Simba kutaendelea kutoa nafasi kwa Tanzania kutoa idadi ya timu zaidi zitakazoshiriki michuano ya kimataifa huku wakizingatia mwongozo uliotolewa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuhusiana na ugonjwa wa corona.

Kiongozi huyo alisema ulinzi utakuwa wa hali ya juu na mashabiki watakaohudhuria mchezo huo wasiwe na wasiwasi wowote.

Kaizef Chiefs iliwasili nchini juzi, lakini kambi ya timu hiyo ikiwa na ulinzi wa hali ya juu kwa ajili ya kujiepusha na hujuma ya aina yoyote.

Golikipa chaguo la kwanza la timu hiyo, Itumeleng Khune ambaye alikosekana katika mechi ya kwanza amejumuisha katika kikosi kilichowasili nchini baada ya kumaliza kutumikia adhabu ya kadi tatu za njano.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9

9 770856 541002 >